# القرآن الحكيم

# QURANI TAKATIFU

Swahili Quran Translation

by
Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy
(Former Chief Kadhi of
Zanzibar & Kenya)

وَهُمْ أَغْنِيَاءُ ۚ رَضُوا بِأَن يَكُونُوا مَعَ الْخَوَالِفِ
وَطَبَعَ اللَّهُ عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ فَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٩٣﴾

kitu), na hali wao ni matajiri, wameridhia kuwa pamoja na wanaobakia nyuma. Na Mwenyezi Mungu amewapiga muhuri juu ya nyoyo zao; kwa hivyo hawajui (lolote wala hawabali).

يَعْتَذِرُونَ إِلَيْكُمْ إِذَا رَجَعْتُمْ إِلَيْهِمْ ۚ قُل لَّا
تَعْتَذِرُوا لَن نُّؤْمِنَ لَكُمْ قَدْ نَبَّأَنَا اللَّهُ مِنْ أَخْبَارِكُمْ ۚ
وَسَيَرَى اللَّهُ عَمَلَكُمْ وَرَسُولُهُ ثُمَّ تُرَدُّونَ إِلَىٰ
عَالِمِ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ فَيُنَبِّئُكُم بِمَا كُنتُمْ
تَعْمَلُونَ ﴿٩٤﴾

94. Watakutoleeni udhuru mtakaporudi (mkakutana nao). Sema: "Msitoe udhuru; hatutakuaminini. Mwenyezi Mungu amekwisha kutueleza khabari zenu. Na karibuni hivi Mwenyezi Mungu ataviona vitendo vyenu (tena) na Mtume Wake (pia). Kisha (mkifa) mtarudishwa kwa Mjuzi wa ya siri na ya dhahiri, naye atakuambieni (yote) yale mliyokuwa mkiyatenda."

سَيَحْلِفُونَ بِاللَّهِ لَكُمْ إِذَا انقَلَبْتُمْ
إِلَيْهِمْ لِتُعْرِضُوا عَنْهُمْ ۖ فَأَعْرِضُوا عَنْهُمْ ۖ إِنَّهُمْ
رِجْسٌ ۖ وَمَأْوَاهُمْ جَهَنَّمُ جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٩٥﴾

95. Watakuapieni Mwenyezi Mungu mtakaporudi kwao (mkakutana nao), ili muwasamehe (myapuze waliyoyafanya). Basi wapuzilieni mbali. Bila shaka wao ni najisi, na makazi yao ni Jahanamu. Ni malipo ya yale waliyokuwa wakiyachuma.

يَحْلِفُونَ لَكُمْ لِتَرْضَوْا عَنْهُمْ ۖ فَإِن تَرْضَوْا عَنْهُمْ
فَإِنَّ اللَّهَ لَا يَرْضَىٰ عَنِ الْقَوْمِ الْفَاسِقِينَ ﴿٩٦﴾

96. Wanakuapieni ili muwe radhi nao. Basi mkiwa radhi nao nyinyi (ndiyo nini maadamu Mwenyezi Mungu hakuwapa radhi?), basi Mwenyezi Mungu hawi radhi na watu wavunjao amri.

الْأَعْرَابُ أَشَدُّ كُفْرًا وَنِفَاقًا وَأَجْدَرُ أَلَّا يَعْلَمُوا
حُدُودَ مَا أَنزَلَ اللَّهُ عَلَىٰ رَسُولِهِ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ
حَكِيمٌ ﴿٩٧﴾

97. Mabedui wamezidi sana katika ukafiri na unafiki na wameelekea zaidi wasijue mipaka ya yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu juu ya Mtume Wake. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi (na) Mwenye hikima.

وَمِنَ الْأَعْرَابِ مَن يَتَّخِذُ مَا يُنفِقُ مَغْرَمًا
وَيَتَرَبَّصُ بِكُمُ الدَّوَائِرَ ۚ عَلَيْهِمْ دَائِرَةُ السَّوْءِ ۗ
وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٩٨﴾

98. Na katika Mabedui hao wako wanaofikiri kuwa wanayoyatoa (katika kusaidia Uislamu) ni gharama ya bure, na wanakungojeleeni misiba. Misiba mibaya itakuwa juu yao (itawafika wao). Na Mwenyezi Mungu ndiye asikiaye na ajuaye.

---

91,92. Wanatajwa wenye kupewa udhuru.

93. Wanatajwa wenye kustahiki lawama.

94. Tumeona katika Aya ya 81 ya Sura hii kuwa vilipoandaliwa vita vya kwenda kupigana na Warumi wale waliokuwa hawana Uislamu wa kweli walijipurukusha wasende. Wakaja wengine kutoa nyudhuru za uwongo, na wengine wakangojea huko vitani.

97. Watu wakikaa katika miji wakakutana na watu hawa na watu hawa wanajua yaliyo mema na yaliyo mabaya. Wanajua haya kwa ile taathira wanayoiona kwa mambo hayo na kwa kusikia.

Lakini watu wakikaa vichungu vidogo vidogo majangwani na maporini na mashambani hawajui haya, kwa hivyo kwao ujinga unabobea na ukaidi. Ndivyo ikaambiwa hapa 'Mabedui wamezidi sana katika ukafiri na unafiki' Na tamko hilo la *'Al Aarab'* siyo kama tamko la *'Al Arab.'* *'Al Arab'*.maana yake Waarabu. Na *Al Aarab* maana yake ni kila asiyekuwa mkazi wa mji, kama vile wakazi wa porini, jangwani, mashambani na kama huko; akiwa Muarabu au Muafrika au Mzungu au Mchina au wa kabila nyingine.

Basi sivyo hivyo wanavyojivurumizia tu hao wanaojidai kufasiri Qurani—na hali ya kuwa hawajui lugha ya Kiarabu — wakaona *Al Arab* na *Al Aarab* ni maana moja na maana yake ni Waarabu. Wakasema kuwa Waarabu wamezidi sana katika ukafiri na unafiki!

Haifai kabisa kwa mtu kuifasiri Qurani pasi na kujua kweli kweli. Mwenyezi Mungu atamtia adabu kubwa

99. Na katika Mabedui hao wako wanaomuamini Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho, na wanaitakidi kuwa wanayoyatoa ndiyo (sababu za) kuwasogeza kwa Mwenyezi Mungu, na za (kupatia) dua za Mtume. Sikieni! Hakika hayo ni (kweli kuwa ni) mambo ya kuwasogeza kwa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu atawaingiza katika rehema Yake. Bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

وَمِنَ الْأَعْرَابِ مَنْ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ
وَيَتَّخِذُ مَا يُنْفِقُ قُرُبَاتٍ عِنْدَ اللَّهِ وَصَلَوَاتِ
الرَّسُولِ ۚ أَلَا إِنَّهَا قُرْبَةٌ لَهُمْ ۚ سَيُدْخِلُهُمُ اللَّهُ
فِي رَحْمَتِهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٩٩﴾

100. Na wale waliotangulia wakawa wa kwanza katika (Uislamu)—Muhajiri na Ansari, na wale waliowafuata kwa mwendo mzuri—Mwenyezi Mungu atawapa radhi, nao wamridhie (Mwenyezi Mungu kwa hayo mazuri atakayowapa) na amewaandalia Mabustani yapitayo mito mbele yake, wakakae humo milele. Huku ndiko kufuzu kukubwa.

وَالسَّابِقُونَ الْأَوَّلُونَ مِنَ الْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنْصَارِ
وَالَّذِينَ اتَّبَعُوهُمْ بِإِحْسَانٍ رَضِيَ اللَّهُ
عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ وَأَعَدَّ لَهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي
تَحْتَهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ۚ ذَٰلِكَ الْفَوْزُ
الْعَظِيمُ ﴿١٠٠﴾

101. Na katika Mabedui wanaokaa pembezoni mwenu katika vitongoji vya karibu yenu hapo Madina) kuna wanafiki. Na katika wenyeji wa Madina (pia kuna wengine wanafiki); wamebobea katika unafiki; (hata) huwajui (kuwa ni wanafiki). Sisi tunawajua. Tutawaadhibu mara mbili, kisha watarudishwa katika adhabu kubwa.

وَمِمَّنْ حَوْلَكُمْ مِنَ الْأَعْرَابِ مُنَافِقُونَ ۖ وَمِنْ أَهْلِ
الْمَدِينَةِ ۖ مَرَدُوا عَلَى النِّفَاقِ لَا تَعْلَمُهُمْ ۖ نَحْنُ
نَعْلَمُهُمْ ۚ سَنُعَذِّبُهُمْ مَرَّتَيْنِ ثُمَّ يُرَدُّونَ إِلَىٰ
عَذَابٍ عَظِيمٍ ﴿١٠١﴾

102. Na (wako) wengine wamekiri dhambi zao (wametubia kwa Mwenyezi Mungu, wakapokelewa). Wamechanganya vitendo vizuri na vingine vibaya. Asaa Mwenyezi Mungu akapokea toba zao. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

وَآخَرُونَ اعْتَرَفُوا بِذُنُوبِهِمْ خَلَطُوا عَمَلًا صَالِحًا
وَآخَرَ سَيِّئًا عَسَى اللَّهُ أَنْ يَتُوبَ عَلَيْهِمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ
غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١٠٢﴾

103. Chukua sadaka katika; mali zao, uwasafishe na kwatakasa kwa ajili ya hizo (sadaka zao) na kuwataja kwa vizuri (mbele yangu) na uwaombee dua. Hakika kuwaombea kwako kutawapa utulivu (watengenekewe); na Mwenyezi Mungu ndiye asikiaye na ajuaye.

خُذْ مِنْ أَمْوَالِهِمْ صَدَقَةً تُطَهِّرُهُمْ وَتُزَكِّيهِمْ بِهَا
وَصَلِّ عَلَيْهِمْ ۖ إِنَّ صَلَاتَكَ سَكَنٌ لَهُمْ ۗ وَاللَّهُ
سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿١٠٣﴾

104. Je! Hawajui ya kwamba Mwenyezi Mungu anapokea toba ya waja Wake na kuzipokea sadaka, na ya kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye kukubali toba sana (na) Mwenye rehema?

أَلَمْ يَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ هُوَ يَقْبَلُ التَّوْبَةَ عَنْ عِبَادِهِ
وَيَأْخُذُ الصَّدَقَاتِ وَأَنَّ اللَّهَ هُوَ التَّوَّابُ
الرَّحِيمُ ﴿١٠٤﴾

---

kabisa ya kumuangamiza kweli kweli Akhera au pengine papa hapa duniani kwani anamsingizia Mwenyezi Mungu asiyoyasema.

100. Malipo watakayoyapata wema—waliotangulia na wa sasa na watakaokuja.

101. Kwenye wema wake mtu na wabaya wake wako, na kwenye wabaya wake na wema wake wapo pia. Kheri tupu kabisa haipatikani. Basi hata huko Madina alikopokewa Mtume namna hiyo kwa kichwa na mikono na miguu, na walikuwa wengine katika hao ni maadui zake kweli kweli, ila wanajidhihirisha tu mbele yake na mbele za watu wake kuwa wao wanamfuata Mtume na kumpenda na kupendelea ya kheri. Kumbe waongo.

105. Na sema (uwaambie): "Tendeni mambo (mazuri). Mwenyezi Mungu atayaona mambo yenu hayo na Mtume Wake na Waislamu. Na mtarudishwa kwa Mjuzi wa siri na dhahiri; naye atakwambieni (yote) mliyokuwa mkiyatenda."

وَقُلِ اعْمَلُوا فَسَيَرَى اللّٰهُ عَمَلَكُمْ وَرَسُولُهُ
وَالْمُؤْمِنُونَ ۚ وَسَتُرَدُّونَ إِلَىٰ عٰلِمِ الْغَيْبِ
وَالشَّهَادَةِ فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٠٥﴾

106. Na wako wengine wanaongojeshwa kwa amri ya Mwenyezi Mungu (bado haijakubaliwa toba yao); ama atawaadhibu au atawapokea. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na Mwenye hikima.

وَاٰخَرُونَ مُرْجَوْنَ لِأَمْرِ اللّٰهِ إِمَّا يُعَذِّبُهُمْ
وَإِمَّا يَتُوبُ عَلَيْهِمْ ۚ وَاللّٰهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿١٠٦﴾

107. Na wako (wanafiki wengine) waliojenga msikiti wa (kuleta) udhia na kutia nguvu ukafiri, na kuwafarikisha walioamini na kuufanya mahali pa kuwangojea wale waliomfanyia vita Mwenyezi Mungu na Mtume wake zamani. Na bila shaka wataapa (waseme): "Hatukukusudia ila wema." Lakini Mwenyezi Mungu anashuhudia kuwa wao ni waongo.

وَالَّذِينَ اتَّخَذُوا مَسْجِدًا ضِرَارًا وَكُفْرًا
وَتَفْرِيقًا بَيْنَ الْمُؤْمِنِينَ وَإِرْصَادًا لِّمَنْ حَارَبَ
اللّٰهَ وَرَسُولَهُ مِنْ قَبْلُ ۚ وَلَيَحْلِفُنَّ إِنْ أَرَدْنَا
إِلَّا الْحُسْنَىٰ ۚ وَاللّٰهُ يَشْهَدُ إِنَّهُمْ لَكٰذِبُونَ ﴿١٠٧﴾

108. Usisimame (msikitini) humo kabisa. Msikiti uliojengwa juu ya msingi wa kumcha Mungu tangu siku ya kwanza (ya kufika Mtume Madina) unastahiki

لَا تَقُمْ فِيهِ أَبَدًا ۚ لَمَسْجِدٌ أُسِّسَ عَلَى التَّقْوٰى مِنْ

---

Wataadhibiwa mara mbili—hapa duniani na kaburini—na kisha wapelekwe katika adhabu kali Akhera.

102-104. Tazama upole wa Mwenyezi Mungu na rehema yake.

106. Itakuja katika Aya ya 118 ya Sura hii hii kuwa Mwenyezi Mungu amewapokea nao, juu ya kitendo chao kibaya kabisa. Na sisi tunaomba tunasema:—

| | |
|---|---|
| Ya uovu ya kudhuru | Tunotenda tufutiye |
| Ni akili kutuduru | Na sheitani si siye |
| Inshallahu maadhuru | Unosamehe ni weye |
| Ilahi tuhurumiye | Iwe kun Fayakunu |

107. Wanafiki wengine kwa kumchukia kwao zaidi Mtume waliagana na makafiri kuwa wao wanafiki watajenga msikiti Madina wawatie humo mashujaa wa kikafiri, kisha wamualike Mtume huko. Akiingia ndani wamvamie wamuue.

Basi wakataka ruhusa kwa Mtume kujenga msikiti mwengine huko Madina mbali kidogo na msikiti mkubwa wa Mtume wa Madina, na Mtume akawapa ruhusa kwani alikuwa hajui azma yao. Na Mwenyezi Mungu akawaachia tu wakukurike na wakhasirike; mpaka msikiti ulipokwisha.

Ulipokwisha Mwenyezi Mungu alimwuamrisha Mtume akauvunje na akazitaja hapa baadhi ya sababu za kuvunja msikiti huo Kuwa wanataka wote pamoja katika msikiti mkubwa wa Mtume. Iwe wengine katika msikiti wa Mtume na wengine wanasali katika msikiti huo mpya. Iwe hakuna kukutana tena wote pamoja kila siku mara tano ila katika siku ya Ijumaa tu na Idi na shughuli kubwa. Na huu sio muradi wa Uislamu kwa kuamrisha kusaliwa jamaa msikitini. Makusudio ya kusaliwa jamaa msikitini iwe Waislamu wanakutana huko kila siku mara tano.

Basi mpaka leo hii inakatazwa mtu kujenga msikiti wake karibu na mahala penye msikiti tangu zamani. Naakajenge mahala ambapo ni mbali na msikiti, hata ikawa watu wa huko wanapata taabu kuufuatia msikiti huo uliokо mbali.

zaidi wewe usimame humo. Humo wamo watu wanaopenda kujitakasa. Na Mwenyezi Mungu anawapenda wajitakasao. (Nao ndio ule msikiti wa Mtume unaosaliwa na Masahaba watahirifu).

أَوَّلِ يَوْمٍ أَحَقُّ أَنْ تَقُومَ فِيهِ ۚ فِيهِ رِجَالٌ
يُحِبُّونَ أَنْ يَتَطَهَّرُوا ۚ وَاللَّهُ يُحِبُّ الْمُطَّهِّرِينَ ﴿١٠٨﴾

109. Je! Aliyeweka msingi wa jengo lake kwa kumuogopa Mwenyezi Mungu na kutaka radhi (Yake), siye bora au aliyeweka msingi wa jengo lake juu ya ukingo wa shimo unaobugujika udongo wake, ukaanguka pamoja naye katika moto wa Jahanamu (ndiye bora)? Na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu madhalimu (yakawaongokea mambo yao).

أَفَمَنْ أَسَّسَ بُنْيَانَهُ عَلَىٰ تَقْوَىٰ مِنَ اللَّهِ وَرِضْوَانٍ
خَيْرٌ أَمْ مَنْ أَسَّسَ بُنْيَانَهُ عَلَىٰ شَفَا جُرُفٍ هَارٍ
فَانْهَارَ بِهِ فِي نَارِ جَهَنَّمَ ۗ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي
الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿١٠٩﴾

110. Jengo lao hilo walilolijenga (likavunjwa na Mtume) litakuwa sababu ya kutia wasiwasi (uchungu) nyoyoni mwao (siku zote), mpaka nyoyo zao zikatike vipande vipande. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi (na) Mwenye hikima.

لَا يَزَالُ بُنْيَانُهُمُ الَّذِي بَنَوْا رِيبَةً فِي قُلُوبِهِمْ إِلَّا
أَنْ تَقَطَّعَ قُلُوبُهُمْ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ع ﴿١١٠﴾

111. Mwenyezi Mungu amenunua kwa Waislamu nafsi zao na mali zao (watoe nafsi zao na mali zao katika kupigania dini) ili na yeye awape Pepo. Wanapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu; wanaua na wanauawa. Hii ndiyo ahadi aliyojilazimisha (Mwenyezi Mungu) katika Taurati na Injili na Qurani. Na ni nani atekelezaye zaidi ahadi yake kuliko Mwenyezi Mungu? Basi furahini kwa biashara yenu mliyofanya naye (Mwenyezi Mungu). Na huko ndiko kufuzu kukubwa.

إِنَّ اللَّهَ اشْتَرَىٰ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ أَنْفُسَهُمْ
وَأَمْوَالَهُمْ بِأَنَّ لَهُمُ الْجَنَّةَ ۚ يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ
اللَّهِ فَيَقْتُلُونَ وَيُقْتَلُونَ ۖ وَعْدًا عَلَيْهِ حَقًّا فِي
التَّوْرَاةِ وَالْإِنْجِيلِ وَالْقُرْآنِ ۚ وَمَنْ أَوْفَىٰ بِعَهْدِهِ
مِنَ اللَّهِ ۚ فَاسْتَبْشِرُوا بِبَيْعِكُمُ الَّذِي بَايَعْتُمْ بِهِ ۚ
وَذَٰلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿١١١﴾

112. (Hao walioahidiwa kupata haya ni wale) wanaotubia (wakikosa), wanaofanya ibada (kweli kweli), wanaomshukuru (Mwenyezi Mungu) wanaofunga, wanaorukuu, na kusujudu (yaani wanaosali), wanaoamrisha yaliyo mema, na wanaokataza yaliyo mabaya, na wanaohifadhi mipaka ya Mwenyezi Mungu; (hawaipindukii). Basi wape habari njema hao walioamini (hivi).

التَّائِبُونَ الْعَابِدُونَ الْحَامِدُونَ
السَّائِحُونَ الرَّاكِعُونَ السَّاجِدُونَ الْآمِرُونَ
بِالْمَعْرُوفِ وَالنَّاهُونَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَالْحَافِظُونَ
لِحُدُودِ اللَّهِ ۗ وَبَشِّرِ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١١٢﴾

---

Lakini watu wanasikia!? Chungu chungu ya misikiti utaona mitaani imekaribiana wala hapana mmoja unaojaa ikawa sababu ya kujenga huo mwengine. Wanajenga kwa ajili ya kutafuta jina tu—Bwana Fulani amejenga na mimi najenga! Kufanya hivi hakumpatishii mtu thawabu kabisa. Thawabu zinapatikana kwa kufanya kitu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu si kwa ajili ya kujitapa na kutaka kusikiwa na watu.

Basi ukavunjwa msikiti wa wanafiki hao. Na ilipotoka amri hiyo ya kuvunjwa ndipo walipotapatapa na kuapa kuwa wamejenga kwa ajili ya kheri si kwa ajili ya shari. Na hali ya kuwa walikuwa wameujenga kwa ajili ya shari. Na kwa ajili ya kuwangojea hao maadui wa Waislamu waje wamuue Mtume.

108. Basi misikiti unayoijua kwa yakini kuwa haikujengwa kwa nia nzuri usiitumie.

Na huo Msikiti 'Uliyojengwa siku ya kwanza ya kufika Mtume Madina' na Msikiti wa Mtume Mashuhuri ulioko mjini Madina na msikiti ulioko katika kiunga cha Madina kinachoitwa Qubaa. Ukisha Msikiti wa Makka wa Al-Kaaba hapana bora zaidi kuliko msikiti wa Madina, khalafu msikiti wa Baitil Muqaddas (Falastini).

Khalafu misikiti yote—iliyojengwa kwa nia nzuri—ni daraja moja. Asijidai mtu kuusifu msikiti wa nchi yake au mji wake au wa mtaa au wa watu wengine, kuwa huo ndio wanne wao, na wa mahala fulani ndio wa Tano wao na . . . Hakusema Mtume maneno hayo. Daraja za misikiti hiyo za ndani anazijua Mwenyewe Mwenyezi Mungu.

113. Haimpasii Mtume na wale walioamini kuwatakia samahani washirikina ijapokuwa ni jamaa (zao); baada ya kuwabainikia kuwa wao ni watu wa (moto wa) Jahanamu.

مَا كَانَ لِلنَّبِيِّ وَالَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا اَنْ يَّسْتَغْفِرُوْا لِلْمُشْرِكِيْنَ وَلَوْ كَانُوْٓا اُولِيْ قُرْبٰى مِنْۢ بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمْ اَنَّهُمْ اَصْحٰبُ الْجَحِيْمِ ﴿١١٣﴾

114. Wala haikuwa Ibrahimu kumtakia samahani baba yake ila kwa sababu ya ahadi aliyofanya naye. Lakini ilipombainikia kwamba yeye (huyo baba yake) ni adui wa (dini ya) Mwenyezi Mungu (kwa ukaidi tu si kwa ujinga), alijiepusha naye. Kwa yakini Ibrahimu alikuwa mwingi wa kurejea kwa Mungu (na) mvumilivu.

وَمَا كَانَ اسْتِغْفَارُ اِبْرٰهِيْمَ لِاَبِيْهِ اِلَّا عَنْ مَّوْعِدَةٍ وَّعَدَهَآ اِيَّاهُ ۚ فَلَمَّا تَبَيَّنَ لَهٗٓ اَنَّهٗ عَدُوٌّ لِّلّٰهِ تَبَرَّاَ مِنْهُ ۗ اِنَّ اِبْرٰهِيْمَ لَاَوَّاهٌ حَلِيْمٌ ﴿١١٤﴾

115. Na haiwi kwa Mwenyezi Mungu kuwahisabu watu kuwa wamepotea baada ya kuwa amewaongoza mpaka awabainishie ya kujiepusha nayo. (Wakikataa kujiepusha nayo ndipo wanapohisabika kuwa ni waovu). Hakika Mwenyezi Mungu anajua kila kitu.

وَمَا كَانَ اللّٰهُ لِيُضِلَّ قَوْمًاۢ بَعْدَ اِذْ هَدٰىهُمْ حَتّٰى يُبَيِّنَ لَهُمْ مَّا يَتَّقُوْنَ ۗ اِنَّ اللّٰهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيْمٌ ﴿١١٥﴾

116. Mwenyezi Mungu anao ufalme wa mbingu na ardhi; huhuisha na kufisha. Nanyi hamna mlinzi wala msaidizi isipokuwa Mwenyezi Mungu.

اِنَّ اللّٰهَ لَهٗ مُلْكُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ۗ يُحْيٖ وَيُمِيْتُ ۗ وَمَا لَكُمْ مِّنْ دُوْنِ اللّٰهِ مِنْ وَّلِيٍّ وَّلَا نَصِيْرٍ ﴿١١٦﴾

117. Bila shaka Mwenyezi Mungu amemuelekea kwa rehema Mtume na Muhajiri na Ansari waliomfuata yeye (Mtume) katika ile saa ya dhiki (wakenda vitani kupigana na Warumi); wakati ambao nyoyo za baadhi yao zilikuwa karibu kugeuka (kufuata ukafiri); basi akawaelekea (Mwenyezi Mungu) kwa rehema. Kwa yakini yeye (Mwenyezi Mungu) kwao ni Mpole (na) Mwenye rehema

لَقَدْ تَّابَ اللّٰهُ عَلَى النَّبِيِّ وَالْمُهٰجِرِيْنَ وَالْاَنْصَارِ الَّذِيْنَ اتَّبَعُوْهُ فِيْ سَاعَةِ الْعُسْرَةِ مِنْۢ بَعْدِ مَا كَادَ يَزِيْغُ قُلُوْبُ فَرِيْقٍ مِّنْهُمْ ثُمَّ تَابَ عَلَيْهِمْ ۗ اِنَّهٗ بِهِمْ رَءُوْفٌ رَّحِيْمٌ ﴿١١٧﴾

118. Na (pia akawaelekea kwa rehema) wale watatu waliongojeshwa (kukubaliwa toba yao kwa yale makosa yao makubwa waliyoyafanya); hata ardhi ikawa dhiki kwao, pamoja na wasaa wake; na nafsi zao zikadhikika juu yao, na wakayakinisha ya kwamba hakuna kwa kumkimbia Mwenyezi Mungu

وَّعَلَى الثَّلٰثَةِ الَّذِيْنَ خُلِّفُوْا ۗ حَتّٰٓى اِذَا ضَاقَتْ عَلَيْهِمُ الْاَرْضُ بِمَا رَحُبَتْ وَضَاقَتْ عَلَيْهِمْ اَنْفُسُهُمْ وَظَنُّوْٓا اَنْ لَّا مَلْجَاَ مِنَ اللّٰهِ اِلَّآ

---

Lakini daraja zao za dhahiri ni sawa. Kwa hivi hata ukiweka nadhiri kusali rakaa mbili katika msikiti fulani isiyokuwa ile mitatu—haikulazimu kwenda kusali katika msikiti huo. Sali msikiti uutakao. Hivi ndivyo vinavyosema vitabu vyetu vyote vya dini. Yaliyosalia ni kujigamba tu kusikokuwa na maana. Na maneno yasiyokuwa na hoja na dalili ni ya kutupwa.

110. Inazidi kutajwa habari ya ule msikiti uliotajwa katika Aya ya 107.

111-112. Wanatajwa Waislamu wa kweli namna wanavyokuwa na namna wanavyofanya na watakayoyapata. Basi na sisi tukifanya hivi tutapata hayo.

113: Mtume na baadhi ya Masahaba walikuwa wanawaombea dua jamaa zao waliokufa katika ukafiri. Basi ndio wanaambiwa hapa kuwa wasiwaombee dua kwani watu hao walikuwa wakijua kuwa Uislamu ni dini ya haki ila walikuwa wakikataa kwa ujeuri na inadi, si kwa kuwa walikuwa hawajui; wakijua—kama majina yao ya utoto—kuwa hayo waliyokuwa wakiambiwa ni haki.

114. Na wakaambiwa katika Aya hii kuwa wasitoe hoja kwa kuwa Nabii Ibrahimu alimuombea dua baba yake, kwani Nabii Ibrahimu aliomba dua hizo alipokuwa akidhani kuwa baba yake ni mjinga—hajui haki wala batili. Lakini ilipombainikia kuwa anajua lakini anafanya ukaidi tu na ushupavu aliacha kumuombea hizo dua. Na huyu ni ami yake.

ila (kuelekea) Kwake, kisha (Mwenyezi Mungu) akawaelekea kwa rehema Yake ili wapate kukubaliwa toba yao. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye apokeaye toba na Mwenye rehema.

إِلَيْهِ ۚ ثُمَّ تَابَ عَلَيْهِمْ لِيَتُوبُوا ۚ إِنَّ اللَّهَ هُوَ التَّوَّابُ
الرَّحِيمُ ﴿١١٨﴾

119. Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu na kuweni pamoja na wakweli (wanaosadikisha Uislamu wao kwa vitendo si kwa maneno tu ya mdomo).

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَكُونُوا مَعَ
الصَّادِقِينَ ﴿١١٩﴾

120. Haikuwapasia watu wa Madina—na Mabedui wakaao pembeni mwao — kubaki nyuma ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (wasende vitani). Wala (haiwapasii) kujipendelea nafsi zao kuliko nafsi yake (Mtume, wakamwacha Mtume kwenda vitani, wao wakasalia na raha zao Madina). Hayo ni kwa sababu ya kuwa hawapatikani na kiu wala taabu wala njaa katika njia ya Mwenyezi Mungu, wala hawakanyagi njia iwachukizayo makafiri, wala hawamtii adui hasara yoyote, ila huandikiwa kitendo chema (kabisa) kwa ajili ya hayo. Hakika Mwenyezi Mungu haharibu ujira wa watendao wema

مَا كَانَ لِأَهْلِ الْمَدِينَةِ وَمَنْ حَوْلَهُم مِّنَ
الْأَعْرَابِ أَن يَتَخَلَّفُوا عَن رَّسُولِ اللَّهِ وَلَا يَرْغَبُوا
بِأَنفُسِهِمْ عَن نَّفْسِهِ ۚ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ لَا يُصِيبُهُمْ
ظَمَأٌ وَلَا نَصَبٌ وَلَا مَخْمَصَةٌ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلَا
يَطَئُونَ مَوْطِئًا يَغِيظُ الْكُفَّارَ وَلَا يَنَالُونَ
مِنْ عَدُوٍّ نَّيْلًا إِلَّا كُتِبَ لَهُم بِهِ عَمَلٌ صَالِحٌ ۚ
إِنَّ اللَّهَ لَا يُضِيعُ أَجْرَ الْمُحْسِنِينَ ﴿١٢٠﴾

121. Wala hawatowi kinachotolewa chochote, kidogo wala kikubwa, wala hawalipiti bonde lolote (katika kwenda vitani) ila wanaandikiwa, ili Mwenyezi Mungu awalipe (malipo) mema ya yale (mambo) waliyokuwa wakiyatenda.

وَلَا يُنفِقُونَ نَفَقَةً صَغِيرَةً وَلَا كَبِيرَةً وَلَا
يَقْطَعُونَ وَادِيًا إِلَّا كُتِبَ لَهُمْ لِيَجْزِيَهُمُ اللَّهُ أَحْسَنَ
مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٢١﴾

122. Wala haiwapasii Waislamu kutoka wote (katika miji yao wakajaa Madina wakaiwacha miji yao mitupu). Lakini kwa nini halitoki kundi (tu) katika kila taifa miongoni mwao (lende Madina kwa Mtume (kujialimisha vyema dini na (kisha wakaja) kuwaonya wenziwao (waliosalia makwao) watakapowarudia, ili wapate kujihadharisha (na wao na mabaya).

وَمَا كَانَ الْمُؤْمِنُونَ لِيَنفِرُوا كَافَّةً ۚ فَلَوْلَا نَفَرَ مِن
كُلِّ فِرْقَةٍ مِّنْهُمْ طَائِفَةٌ لِّيَتَفَقَّهُوا فِي الدِّينِ
وَلِيُنذِرُوا قَوْمَهُمْ إِذَا رَجَعُوا إِلَيْهِمْ لَعَلَّهُمْ
يَحْذَرُونَ ﴿١٢٢﴾

---

115. Hapa wanatulizwa nyoyo zao wasione kuwa wamefanya vibaya katika huko kuwaombea dua hao wazee wao makafiri, kwani walikuwa bado hawajakatazwa jambo hilo; na maadamu bado jambo halijakatazwa hapana madhambi katika kulifanya.

118. Watu hao ni wale wale iliyotajwa habari yao katika Aya ya 106 wakaambiwa kuwa kunangojeshwa bado kukubaliwa toba yao. Hapa inatajwa kuwa sasa imekwisha kukubaliwa baada ya yale majonzi na huzuni iliyowapata kwa kujuta kwa yale makosa yao. Nao ni Mabwana wakubwa hao:

(a) Bwana Hilal bin Umayya Al Ansary Al Awsy;
(b) Bwana Murara bin Rabii Al Ansary Al Awsy;
(c) Bwana Kaab bin Malik Al Ansary Al Khazrajy.

120-121. Wanatahayarishwa baadhi ya Waislamu wa zama hizo waliokuwa wakizikhitaria nafsi zao raha na kumwachia Mtume taabu. Sivyo hivyo. Unayempenda mchukulie wewe taabu zake sio yeye akuchukulieni taabu zenu. Si mapenzi hayo bila ya shaka.

Na wanatajiwa thawabu watakazozipata watakapochukua taabu hizo. Asali haiwezi kupatikana bila ya kupigwa na misumari ya nyuki. Chuma juani ndipo ule kivulini; au utakufa njaa.

122. Masahaba—kwa hima kubwa yao ya kutaka kujua dini na kutaka kutwa kucha wawe pamoja na Mtume

123. Enyi mlioamini. Piganeni na wale makafiri walio karibu yenu (kwanza kwani ndio wenye madhara na nyinyi zaidi) na waukute ugumu kwenu (msilegee, mpigane nao barabara hata wajue kuwa wamekutana na wanaume kweli kweli, waogope kukuoneeni tena). Na jueni ya kwamba Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanaomuogopa (kama nyinyi hivi, kwa hiyo atakunusuruni juu yao).

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا قَاتِلُوا الَّذِينَ يَلُونَكُم مِّنَ الْكُفَّارِ وَلْيَجِدُوا فِيكُمْ غِلْظَةً ۚ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ مَعَ الْمُتَّقِينَ ﴿١٢٣﴾

124. Na inapoteremshwa sura (mpya ya Qurani) wako miongoni mwao (watu wanafiki) wasemao: "Ni nani miongoni mwenu (sura) hii imemzidishia imani?" Ama wale walioamini inawazidishia imani, nao wanafurahi.

وَإِذَا مَا أُنزِلَتْ سُورَةٌ فَمِنْهُم مَّن يَقُولُ أَيُّكُمْ زَادَتْهُ هَٰذِهِ إِيمَانًا ۚ فَأَمَّا الَّذِينَ آمَنُوا فَزَادَتْهُمْ إِيمَانًا وَهُمْ يَسْتَبْشِرُونَ ﴿١٢٤﴾

125. Ama wale wenye ugonjwa nyoyoni mwao, basi inawazidishia ubaya (mpya) juu ya ubaya waliokuwa nao; na wanakufa na hali ni makafiri.

وَأَمَّا الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٌ فَزَادَتْهُمْ رِجْسًا إِلَىٰ رِجْسِهِمْ وَمَاتُوا وَهُمْ كَافِرُونَ ﴿١٢٥﴾

126. Je! Hawaoni ya kwamba wanatiwa mtihanini kila mwaka mara moja au mara mbili (au zaidi)? Kisha hawatubu wala hawakumbuki.

أَوَلَا يَرَوْنَ أَنَّهُمْ يُفْتَنُونَ فِي كُلِّ عَامٍ مَّرَّةً أَوْ مَرَّتَيْنِ ثُمَّ لَا يَتُوبُونَ وَلَا هُمْ يَذَّكَّرُونَ ﴿١٢٦﴾

127. Na inapoteremshwa sura (mpya huwa) wanatazamana (hao wanafiki) wao kwa wao (ili wapate kukimbia wasisikie maneno hayo, na huku wanakonyezana kuambiana): "Je! yuko yoyote anayekuoneni?" (Wanaulizana hivi ili wakimbie). Kisha hugeuka wakakimbia. Mwenyezi Mungu amezigeuza nyoyo zao kwa kuwa wao ni watu wasiotaka kufahamu.

وَإِذَا مَا أُنزِلَتْ سُورَةٌ نَّظَرَ بَعْضُهُمْ إِلَىٰ بَعْضٍ هَلْ يَرَاكُم مِّنْ أَحَدٍ ثُمَّ انصَرَفُوا ۚ صَرَفَ اللَّهُ قُلُوبَهُم بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَّا يَفْقَهُونَ ﴿١٢٧﴾

128. Amekufikieni Mtume aliye jinsi moja na nyinyi, yanamuhuzunisha yanayokutaabisheni, anakuhangaikieni. (Na) kwa walioamini ni mpole na Mwenye huruma.

لَقَدْ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مِّنْ أَنفُسِكُمْ عَزِيزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ حَرِيصٌ عَلَيْكُم بِالْمُؤْمِنِينَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿١٢٨﴾

129. Na kama wakidumu kukengeuka (hao makafiri) sema: "Mwenyezi Mungu atanitoshea (atanikifia balaa yenu), hakuna wa kuabudiwa ila Yeye tu; namtegemea Yeye, naye ndiye Mola wa (hiyo) Arshi iliyo kubwa (kabisa)."

فَإِن تَوَلَّوْا فَقُلْ حَسْبِيَ اللَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ۖ عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ ۖ وَهُوَ رَبُّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ ﴿١٢٩﴾

— walikuwa wanaacha miji yao wakisilimu wanakuja wote kukaa Madina. Wakakatazwa hayo isije ikafa hiyo miji isije Madina isiweze kuwachukua wote. Hauwezi mji mmoja kuchukua watu wa chungu ya miji. Basi ikaambiwa kuwa wawe wakija baadhi ya watu tu katika kila miji.

123. Ikiwa una maadui walio khatari kwako, muanze aliye karibu yako, umlaze vizuri, waogope walio mbali; ipatikane salama.

124-127. Vinatajwa baadhi ya vitendo vibaya vya wanafiki na yanayowafika. Nao wameshika pale pale walipo.

128. Hapa zinatajwa baadhi ya sifa za Mtume Muhammad (s.a.w.) kuwa yeye kwa umma wake ni kama mzazi: (a) Anataabika akihisi kuwa umma wake unataabika au utataabika; (b) Ana pupa utengenee upesi upesi; (c,d) Ana rehema na huruma juu yao.

Al Muradi ni kama Mzee na Watoto wake.

129. Wanaambiwa Waislamu wasiwajali hao wabaya. Wamtegemee Mwenyezi Mungu, wafanye yapasayo. Wakati mwengine sharti ifuatwe kawaida hii: Akutendaye Mtende, Mche Asiyekutenda.

Ina Aya 109

# SURAT YUNUS

Ina Makaro 11

*(Imeteremka Makka)*

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

الٓرٰ ۚ تِلْكَ اٰيٰتُ الْكِتٰبِ الْحَكِيْمِ ①

Alif Lam Ra. Hizi ni Aya za Kitabu chenye hikima.

أَكَانَ لِلنَّاسِ عَجَبًا أَنْ أَوْحَيْنَآ إِلٰى رَجُلٍ مِّنْهُمْ
أَنْ أَنْذِرِ النَّاسَ وَبَشِّرِ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْٓا أَنَّ لَهُمْ
قَدَمَ صِدْقٍ عِنْدَ رَبِّهِمْ ۗ قَالَ الْكٰفِرُوْنَ إِنَّ
هٰذَا لَسِحْرٌ مُّبِيْنٌ ②

2. Je! Ni ajabu kwa watu ya kwamba tumemfunulia (tumemletea Wahyi) mtu miongoni mwao kuwa: "Waonye watu na wape walioamini habari njema ya kwamba watakuwa na cheo kikubwa mbele ya Mola wao?" Wakasema makafiri: "Hayakuwa haya ila ni kiini macho."

إِنَّ رَبَّكُمُ اللّٰهُ الَّذِيْ خَلَقَ السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضَ فِيْ
سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوٰى عَلَى الْعَرْشِ يُدَبِّرُ الْأَمْرَ ۖ مَا
مِنْ شَفِيْعٍ إِلَّا مِنْۢ بَعْدِ إِذْنِهٖ ۚ ذٰلِكُمُ اللّٰهُ رَبُّكُمْ
فَاعْبُدُوْهُ ۚ أَفَلَا تَذَكَّرُوْنَ ③

3. Bila shaka Mola wenu ni Mwenyezi Mungu ambaye ameziumba mbingu na ardhi katika siku sita. Kisha akatawala juu ya Arshi (yake). Yeye ndiye anayepitisha mambo yote. Hakuna muombezi ila baada ya idhini yake (Mungu). Huyu ndiye Mwenyezi Mungu, Mola wenu, Basi Muabuduni Yeye. Je! hamkumbuki (kuwa hayo mliyo nayo siyo mambo ya haki)?

---

2. Kuja Mtume—kabla ya Nabii Muhammad—si ajabu. Basi tu, wanajitia pambani kwa jambo walijualo. Muhali kupewa mtu Utume baada ya Nabii Muhammad kama alivyosema Mwenyewe Mwenyezi Mungu na Mtume.

3. Katika hii Aya waliyoifanya ya 4 wamejaza chungu ya maneno ya upotezaji katika kulipotoa tamko la *Arsh*. Basi tusighurike na uwongo huo. *Arsh* ni Umbo la Kimbinguni, kubwa zaidi kuliko Mbingu tunazozisikia, lakini viumbe hawawezi kujua hakika yake. Na Ilimu tuliyopewa sisi Binaadamu kikomo chake kidogo kabisa, kama anavyosema Mwenyezi Mungu katika Aya ya 85 ya *Surat Bani Israil*. Basi *Arsh* ya Mwenyezi Mungu si kama walivyosema wao kuwa: "Neno hili linaonyesha sifa zilizo bora za Mwenyezi Mungu."

Mwenyezi Mungu amelitumia katika Qurani tamko la *Arsh* katika KUMKHUSU yeye mara 19. Na hapana mara moja katika hizo ila inaonyesha kuwa hiyo *Arsh* ni kitu kilichoumbwa na Mwenyezi Mungu si sifa Yake.

*(i)* Katika *Stawaa Alal Arsh* mara 7. Katika Aya ya 54 ya *Suratul Aaraf*, Aya ya 3 ya *Surat Yunus*, Aya ya 2 ya *Suratur Raad*, Aya ya 59 ya *Suratul Furqan*, Aya ya 4 ya *Surat Alif Lam Sajdq*, na Aya ya 4 ya *Suratul Hadyd* na Aya 5 ya *Surat Taha*.

*(ii)* Katika *Rabbul Arsh* (Muumba wa hiyo *Arsh tukufu*) mara 4. Katika Aya ya 129 ya *Suratut Tawba* katika Aya ya 2 ya *Suratul Anbiyaa*, Aya ya 86 ya *Suratul Muuminuuna* na Aya ya 82 ya *Suratuz Zukhruf*.

*(iii)* Katika *Dhul Arsh* (Mwenye hiyo *Arsh* tukufu mara 4. Katika Aya ya 42 ya *Surat Bani Israil*, Aya ya 15 ya *Surat Muumin*, Aya ya 20 ya *Suratut Takwyr*, na Aya ya 15 ya *Suratul Buruuj*.

*(iv)* Katika *Yahmilu Arsh* (Wanachukua = Wanaihifadhi = Wanaiendeshea mambo yake) mara 2. Katika Aya ya 7 ya *Suratul Muumin* na Aya ya 17 ya *Suratul Haaqqa*.

*(v)* Katika *Hawlil Arsh* (Pembezoni mwa hiyo *Arsh*) mara 1. Katika Aya ya 75 ya *Suratuz Zumar*.

*(vi)* Katika *Arshuhuu Alal Maai* (Ilikuwa *Arsh* yake juu ya maji) mara moja. Katika Aya ya 7 ya *Surat Huud*.

Natutahadhari na mapotezo yao; wanayoyaita maelezo, kumbe mapotezo. Basi yote hayo waliyoyajaza hapo ni mapotezo; na tafsiri ya hizo Sura walizozitaja siyo; kama hivyo kusema kuwa hilo tamko la *Thamaniya* ni sifa 8; ni

إِلَيْهِ مَرْجِعُكُمْ جَمِيعًا ۖ وَعْدَ اللَّهِ حَقًّا ۚ إِنَّهُ يَبْدَأُ
الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ لِيَجْزِيَ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا
الصَّالِحَاتِ بِالْقِسْطِ ۚ وَالَّذِينَ كَفَرُوا لَهُمْ شَرَابٌ مِنْ
حَمِيمٍ وَعَذَابٌ أَلِيمٌ بِمَا كَانُوا يَكْفُرُونَ ﴿٤﴾

4. Kwake ndiyo marejeo yenu nyote. Hii ni ahadi ya Mwenyezi Mungu iliyo ya kweli. Hakika Yeye ndiye aliyeanzisha Viumbe na ndiye atakayewarejesha (baada ya kufa kwao) ili awalipe kwa uadilifu wale walioamini na kufanya vitendo vizuri. Na waliokufuru, wao watapata vinywaji vya maji yanayochemka na adhabu inayoumiza kwa sababu ya kukataa kwao.

هُوَ الَّذِي جَعَلَ الشَّمْسَ ضِيَاءً وَالْقَمَرَ نُورًا وَ
قَدَّرَهُ مَنَازِلَ لِتَعْلَمُوا عَدَدَ السِّنِينَ وَ
الْحِسَابَ ۚ مَا خَلَقَ اللَّهُ ذَٰلِكَ إِلَّا بِالْحَقِّ ۚ يُفَصِّلُ
الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿٥﴾

5. Yeye (Mwenyezi Mungu) ndiye aliyelifanya jua kuwa muanga, na mwezi kuwa nuru, na akaupimia vituo (huo mwezi) ili mjue idadi ya miaka na hisabu (nyinginezo). Mwenyezi Mungu hakuviumba hivyo ila kwa haki. Anapambanua Aya (zake) kwa watu wanaotaka kujua.

إِنَّ فِي اخْتِلَافِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ وَمَا خَلَقَ اللَّهُ
فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يَتَّقُونَ ﴿٦﴾

6. Hakika katika mfuatano (wa daima) wa usiku na mchana; na katika alivyoviumba Mwenyezi Mungu katika mbingu na ardhi; ziko dalili (dhahiri za kuwa Mwenyezi Mungu ni mmoja tu) kwa watu wanaoogopa.

إِنَّ الَّذِينَ لَا يَرْجُونَ لِقَاءَنَا وَرَضُوا بِالْحَيَاةِ الدُّنْيَا
وَاطْمَأَنُّوا بِهَا وَالَّذِينَ هُمْ عَنْ آيَاتِنَا غَافِلُونَ ﴿٧﴾

7. Hakika wale wasioogopa kukutana nasi, na wakawa radhi na maisha ya dunia na wakatua kwa hayo, na wale wanaoghafilika na Aya zetu

أُولَٰئِكَ مَأْوَاهُمُ النَّارُ بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٨﴾

8. (Wote) Hao makazi yao ni Motoni kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyachuma.

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ يَهْدِيهِمْ رَبُّهُمْ
بِإِيمَانِهِمْ ۖ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهِمُ الْأَنْهَارُ فِي جَنَّاتِ
النَّعِيمِ ﴿٩﴾

9. Hakika wale walioamini na kufanya vitendo vizuri, Mola wao atawaongoza kwa sababu ya imani yao (wende katika Pepo). Itakuwa inapita mito mbele yao, katika (hayo) Mabustani yenye neema.

دَعْوَاهُمْ فِيهَا سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ وَتَحِيَّتُهُمْ فِيهَا سَلَامٌ ۚ
وَآخِرُ دَعْوَاهُمْ أَنِ الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٠﴾

10. Ibada yao humo itakuwa (kusema *subhanakallahumma:* "Utakatifu ni Wako, Ee Mwenyezi Mungu." Na maamkiano yao humo ni (kusema) *salaamun (Alaykum).* Na dua yao ya mwisho (ya kushukuria) ni (kusema; *Alhamdu Lillahi Rabil Alamin)* "Sifa zote njema zinamstahikia Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu wote."

وَلَوْ يُعَجِّلُ اللَّهُ لِلنَّاسِ الشَّرَّ اسْتِعْجَالَهُمْ بِالْخَيْرِ

11. Na kama Mwenyezi Mungu angaliwapa watu upesi upesi shari (wanayojihimizia iwafike), kama wanavyojihimizia kuletewa kheri, bila shaka

---

uwongo kabisa; na kila mwenye kujua nahau ya lugha ya Kiarabu—japo kidogo hivi—anajua kuwa haimkiniki kwa hili tamko la *Thamaniya* kuwa ni *Naatu* ya Sifa. Na wao inamkinika kuwa wanajua; lakini wanataka tu Kuwanga na Jua.

wangalitimiziwa muda wao (mara moja wakajifilia mbali). Basi wale wasioogopa kukutana na Sisi tunawaacha katika upotofu (upotevu) wao wahangaike ovyo.

12. Na dhara inapomgusa mtu huwa anatuomba tu katika (kila hali). Anapolala ubavu, anapokaa na anaposimama. Lakini tunapomuondolea dhara yake hupita (akafanya yake ayatakayo) kama kwamba hakuwa akituomba tumuondoshee dhara iliyompata. Namna hivi wamepambiwa wapitao mipaka yale waliyokuwa wakiyatenda.

13. Na kwa yakini tumekwisha ziangamiza uma nyingi kabla yenu, zilipofanya mabaya; na waliwajia Mitume wao kwa hoja waziwazi; lakini hawakuwa wenye kuamini. Namna hivi tunawalipa watu wanaofanya uovu.

14. Kisha tukakufanyeni nyinyi ndio wenye kushika mahala pao baada ya (kuangamizwa) hao katika ardhi ili tuone jinsi mtakavyotenda.

15. Na wanaposomewa Aya zetu zilizo wazi, wale wasioogopa kukutana nasi husema: "Lete Qurani isiyokuwa hii (ambayo haitatukataza haya tunayoyapenda), au ibadilishe (kidogo hii)." Sema: "Siwezi kuibadilisha kwa khiari ya nafsi yangu; sifuati ila yanayofunuliwa kwangu (ninayoletewa Wahyi). Hakika mimi naogopa—nikimuasi Mola wangu,—adhabu ya Siku (hiyo) iliyo kuu."

16. Sema: "Kama Mwenyezi Mungu angalitaka nisingalikusomeeni hii (Qurani), wala asingalikujulisheni (hiyo Qurani). Nalikaa baina yenu umri (mwingi) kabla ya haya; (hamkunisikia kusema kitu). Basi hamfahamu (kuwa haya si yangu mwenyewe kwa nafsi yangu)?"

لَقُضِيَ إِلَيْهِمْ أَجَلُهُمْ ۖ فَنَذَرُ الَّذِينَ لَا يَرْجُونَ
لِقَاءَنَا فِي طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿١١﴾
وَإِذَا مَسَّ الْإِنسَانَ الضُّرُّ دَعَانَا لِجَنبِهِ أَوْ قَاعِدًا
أَوْ قَائِمًا فَلَمَّا كَشَفْنَا عَنْهُ ضُرَّهُ مَرَّ كَأَن
لَّمْ يَدْعُنَا إِلَىٰ ضُرٍّ مَّسَّهُ ۚ كَذَٰلِكَ زُيِّنَ لِلْمُسْرِفِينَ مَا
كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٢﴾
وَلَقَدْ أَهْلَكْنَا الْقُرُونَ مِن قَبْلِكُمْ لَمَّا ظَلَمُوا ۙ وَ
جَاءَتْهُمْ رُسُلُهُم بِالْبَيِّنَاتِ وَمَا كَانُوا لِيُؤْمِنُوا ۚ
كَذَٰلِكَ نَجْزِي الْقَوْمَ الْمُجْرِمِينَ ﴿١٣﴾
ثُمَّ جَعَلْنَاكُمْ خَلَائِفَ فِي الْأَرْضِ مِن بَعْدِهِمْ
لِنَنظُرَ كَيْفَ تَعْمَلُونَ ﴿١٤﴾
وَإِذَا تُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ آيَاتُنَا بَيِّنَاتٍ ۙ قَالَ الَّذِينَ
لَا يَرْجُونَ لِقَاءَنَا ائْتِ بِقُرْآنٍ غَيْرِ هَٰذَا
أَوْ بَدِّلْهُ ۚ قُلْ مَا يَكُونُ لِي أَنْ أُبَدِّلَهُ مِن تِلْقَاءِ
نَفْسِي ۖ إِنْ أَتَّبِعُ إِلَّا مَا يُوحَىٰ إِلَيَّ ۖ إِنِّي أَخَافُ إِنْ
عَصَيْتُ رَبِّي عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿١٥﴾
قُل لَّوْ شَاءَ اللَّهُ مَا تَلَوْتُهُ عَلَيْكُمْ وَلَا أَدْرَاكُم
بِهِ ۖ فَقَدْ لَبِثْتُ فِيكُمْ عُمُرًا مِّن قَبْلِهِ ۚ
أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿١٦﴾

---

7. Inatajwa hapa khatari ya kuipapia dunia tu tukaitupa Akhera ndiyo nguzo ya KWEGEMA.

11. Watu wakifikwa na taabu mara hujiapiza wakajitakia kufa, lakini Mwenyezi Mungu hachukui dua hizo kama anavyosema hapa.

Na vile vile wanayowaapiza wenzao Mungu hayasikilizi yakiwa si ya haki.

12. Binaadamu mtete na mwizi wa fadhila. Akifikwa kidogo tu hivi hajitambui—madua haya na madua haya na kunyenyekea kwa Mungu. Akitengenekewa tu, mara huyo kamtupilia mbali Mwenyezi Mungu, hana haja naye, utadhani siye yeye.

14. Hapa ulimwenguni ni mahala pa mtihani—ufuzu ukastarehe huko au ufeli ukasumbuke huko. Sumbuka hapa uchukue zawadi huko; ustarehe.

| | |
|---|---|
| Safari ni ndefu | Ndia baidi |
| Si ya mtu kwenda | Aso zawadi |
| Sumbuko la ndia | Likishitadi |
| Huchelewa kuwa | Mtu wa nyuma |
| Zawadi ni zipi | Za kutungata |
| Zilizali hizo | Hukuzipita |
| Zuhudi ya taa | Hukuipata |
| Mbona upumbee | Buna Adama. |

17. Basi ni nani dhalimu zaidi kuliko yule amtungiaye Mwenyezi Mungu uwongo, na akadhibishaye Aya zake? Hakika hawafaulu wale wafanyao maovu.

فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا أَوْ كَذَّبَ بِآيَاتِهِ ۚ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ الْمُجْرِمُونَ ﴿١٧﴾

18. Nao wanaabudu (waungu)—wasiokuwa Mwenyezi Mungu—wasioweza kuwadhuru (wanapoacha kuwaabudu) wala kuwanufaisha (wakiwaabudu). Na wanasema: "Hao (waungu wadogo washirika wake tunaowaabudu) ndio waombezi wetu mbele ya Mwenyezi Mungu." Sema: "Je! Mnamwambia Mwenyezi Mungu asiyoyajua katika mbingu wala katika ardhi?" (Nayo ni kuwa ana washirika. Hayajui haya Mwenyezi Mungu Mwenyewe). Ameepukana na upungufu (wa kutaka mshirika), na ametukuka na hao wanaowashirikisha naye.

وَيَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَضُرُّهُمْ وَلَا يَنفَعُهُمْ وَيَقُولُونَ هَٰؤُلَاءِ شُفَعَاؤُنَا عِندَ اللَّهِ ۚ قُلْ أَتُنَبِّئُونَ اللَّهَ بِمَا لَا يَعْلَمُ فِي السَّمَاوَاتِ وَلَا فِي الْأَرْضِ ۚ سُبْحَانَهُ وَتَعَالَىٰ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿١٨﴾

19. Wala watu hawakuwa (huko nyuma kabisa katika zama za Nabii Adamu) ila kundi moja, (wote wanafuata dini ya haki). Kisha wakahitalifiana. Na kama si neno lililotangulia kutoka kwa Mola wako (kuwa atawalipa siku ya Kiama, hawalipi hapa); bila shaka shauri lao ingekwishakatwa (mara moja) baina yao, katika yale wanayohitalifiana.

وَمَا كَانَ النَّاسُ إِلَّا أُمَّةً وَاحِدَةً فَاخْتَلَفُوا ۚ وَلَوْلَا كَلِمَةٌ سَبَقَتْ مِن رَّبِّكَ لَقُضِيَ بَيْنَهُمْ فِيمَا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ﴿١٩﴾

20. Na wanasema: "Kwa nini haikuteremshwa juu yake kutoka kwa Mola wake miujiza (tunayoitaka)?" Basi sema: "Ilimu ya mambo yasiyoonekana iko kwa Mwenyezi Mungu. Basi ngojeni; na mimi ni pamoja nanyi katika wanaongoja."

وَيَقُولُونَ لَوْلَا أُنزِلَ عَلَيْهِ آيَةٌ مِّن رَّبِّهِ ۖ فَقُلْ إِنَّمَا الْغَيْبُ لِلَّهِ فَانتَظِرُوا إِنِّي مَعَكُم مِّنَ الْمُنتَظِرِينَ ﴿٢٠﴾

21. Na tunapowaonjesha watu rehema baada ya shida iliyowapata, mara huanza kutunga hila za (kutaka kupinga) Aya Zetu. Sema: "Mwenyezi Mungu ni Mwepesi (kabisa) wa kuzipindua hila (zao)." Hakika wajumbe wetu (Malaika) wanaandika hila (zote) wanazozifanya.

وَإِذَا أَذَقْنَا النَّاسَ رَحْمَةً مِّن بَعْدِ ضَرَّاءَ مَسَّتْهُمْ إِذَا لَهُم مَّكْرٌ فِي آيَاتِنَا ۚ قُلِ اللَّهُ أَسْرَعُ مَكْرًا ۚ إِنَّ رُسُلَنَا يَكْتُبُونَ مَا تَمْكُرُونَ ﴿٢١﴾

---

16. Wanasusuwikwa Maqureshi wanaambiwa 'Akalikwakara Kwakwa. Wamezua hilo, na Jingine Tena.' Wanasema kuwa Mtume ameizua hii Qurani, na hali ya kuwa wamekaa naye muda wa miaka arubaini hawakumuwona na mambo ya kutunga wala kukhutubu wala kujibizana wala kushindana katika mambo ya dini wala mengineyo.

Au Kiarabu hiki cha Qurani yuko Binadamu anayeweza kukiandika au kukisema?

Madhalimu kweli hawa — kama ilivyo katika Aya ya 17 — wa nafsi zao na kuwadhulumu viumbe wengine wanaowapoteza makusudi.

Katika maelezo ya hii Aya waliyoifanya ya 17 wamepachikiapachikia ili wamdaie Utume mtu wao. Na ukafiri huu; tumeuvunja katika maelezo ya Aya ya 7 ya *Suratul Faatiha* na Aya ya 4 ya *Suratul Baqarah,* na pia katika Aya ya 115 ya *Suratul Baqarah.*

18. Wanaonyeshwa kuwa tamaa yao hiyo itawatamauka siku ya Kiama.

19. Ubaya wao zaidi ni kuwa wanapokhitalifiana hivyo, wakaletewa Mitume wa kuwatoa katika hizo khitilafu na kuwaongoa, hawakubali kufuata. Hushika pale pale walipo.

20. Hiki ni kisingizio tu chao kusema "Mbona haleti muujiza huu na muujiza huu . . ." Hawataki tu

22. Yeye ndiye anayekuendesheni katika bara na bahari. Hata mnapokuwa katika majahazi na yanakwenda nao kwa upepo mzuri na wakafurahi nao; mara upepo mkali unayajia na mawimbi yanawajia kutoka kila upande, na wanaanza kufikiri ya kwamba wametingwa. (Hapo ndipo) wanapomuomba Mwenyezi Mungu kwa kumtakasia utii, (wakisema): "Ukituokoa katika haya, bila shaka tutakuwa miongoni mwa wanaoshukuru."

هو الذي يسيركم في البر والبحر حتى إذا
كنتم في الفلك وجرين بهم بريح طيبة
وفرحوا بها جاءتها ريح عاصف وجاءهم
الموج من كل مكان وظنوا أنهم أحيط
بهم دعوا الله مخلصين له الدين لئن أنجيتنا
من هذه لنكونن من الشاكرين ﴿٢٢﴾

23. Lakini anapowaokoa, mara wanafanya jeuri (tena) katika ardhi bila haki. "Enyi watu! Jeuri zenu zitakudhuruni wenyewe. Ni starehe (chache tu) za maisha ya dunia, kisha marejeo yenu yatakuwa kwetu. Hapo tutakuambieni (yote) mliyokuwa mkiyafanya."

فلما أنجاهم إذا هم يبغون في الأرض بغير الحق
يا أيها الناس إنما بغيكم على أنفسكم متاع
الحياة الدنيا ثم إلينا مرجعكم فننبئكم
بما كنتم تعملون ﴿٢٣﴾

24. Hakika mfano wa maisha ya dunia (na starehe zake namna zinavyoondoka) ni kama maji tuliyoyateremsha kutoka mawinguni; kisha mimea ya ardhi wanayoila watu na wanyama ikachanganyika nayo (maji hayo, ikastawi). Hata ardhi ilipokamilisha uzuri wake na ikapambika, na wenyewe wakadhani kwamba wao wana uweza juu yake (wakuyavuna na kuyala), mara amri Yetu iliijia usiku au mchana na tukaifanya kama iliyofyekwa, kama kwamba haikuwako jana. Namna hivi tunawaeleza aya (zetu wakazifahamu) watu wanaofikiri.

إنما مثل الحياة الدنيا كماء أنزلناه من
السماء فاختلط به نبات الأرض مما يأكل
الناس والأنعام حتى إذا أخذت الأرض
زخرفها وازينت وظن أهلها أنهم قادرون
عليها أتاها أمرنا ليلا أو نهارا فجعلناها
حصيدا كأن لم تغن بالأمس كذلك نفصل
الآيات لقوم يتفكرون ﴿٢٤﴾

25. Na Mwenyezi Mungu anaweta (viumbe vyake wende) katika (hiyo) nyumba ya amani, na humuongoa amtakaye njia iliyonyoka (maadamu anakubali uwongofu).

والله يدعو إلى دار السلام ويهدي من يشاء
إلى صراط مستقيم ﴿٢٥﴾

26. Wale waliofanya wema watapata (jaza ya) wema (wao) na zaidi; na vumbi halitawafunika nyuso zao wala hawatapatikana na) udhalili. Hao ndio watu wa Peponi; humo watakaa milele.

للذين أحسنوا الحسنى وزيادة ولا يرهق وجوههم
قتر ولا ذلة أولئك أصحاب الجنة هم فيها
خالدون ﴿٢٦﴾

---

kufuata. Huko ni kujitoa kimasomaso tu.

21. Mara nyingi kabisa Mwenyezi Mungu anabainisha wizi wa fadhila wa binadamu, wala si kwa Mwenyezi Mungu tu bali hata kwa wanaadamu wenziwe. Malaimu kila wakifanyiwa wema ndipo wanapolipa ubaya. Na kila aliyewafanyia wema zaidi ndiye wanayemlipa uovu zaidi. Asiwe Mwislamu katika sifa hizo. Hizo sifa za wanyama waovu kama nyoka na walio kama hawa. Ama wanyama wengine—hata walio najisi, kama mbwa—hawana sifa hii mbovu waliyo nayo baadhi ya wanaadamu, na wengine—ati Waislamu. Waislamu. Waislamu! Hao aibu ya Waislamu. Dowa Baya kabisa, katika nguo safi kabisa, nzuri mno kabisa, ya Uislamu. Nawatafadhali waache.

22-23. Kuonyesha vile vile wizi wao wa fadhila.

24. Kuonyesha namna ulimwengu unavyomkolea mtu vizuri, kisha ukamtoka mara moja. Basi tusighuruke na dunia. Dunia ina ghururi. Dunia doo Rang.

Ayyuhal maghururi  Ina khadaa dunia.

25. Tumebainisha katika Aya ya 125 ya *Suratul An-Am* kuwa Mwenyezi Mungu anawaongoa wanaokubali

وَالَّذِينَ كَسَبُوا السَّيِّئَاتِ جَزَاءُ سَيِّئَةٍ بِمِثْلِهَا وَتَرْهَقُهُمْ ذِلَّةٌ ۖ مَا لَهُم مِّنَ اللَّهِ مِنْ عَاصِمٍ ۖ كَأَنَّمَا أُغْشِيَتْ وُجُوهُهُمْ قِطَعًا مِّنَ اللَّيْلِ مُظْلِمًا ۚ أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ ۖ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٢٧﴾

27. Na wale waliochuma maovu, malipo ya uovu ni mfano wake vile vile; (basi watalipwa) na udhalili utawafika. Hawatakuwa na awezaye kuwalinda na (adhabu ya) Mwenyezi Mungu. Zitakuwa nyuso zao kama kwamba zimefudikiziwa vipande vya usiku wenye giza kubwa (yaani zitasawidika nyuso zao kweli kweli). Hao ndio watu wa Motoni; humo watakaa daima.

وَيَوْمَ نَحْشُرُهُمْ جَمِيعًا ثُمَّ نَقُولُ لِلَّذِينَ أَشْرَكُوا مَكَانَكُمْ أَنتُمْ وَشُرَكَاؤُكُمْ ۚ فَزَيَّلْنَا بَيْنَهُمْ ۖ وَقَالَ شُرَكَاؤُهُم مَّا كُنتُمْ إِيَّانَا تَعْبُدُونَ ﴿٢٨﴾

28. Na (wakumbushe) siku tutakapowakusanya wote, kisha tutawaambia wale waliomshirikisha Mungu; "simameni mahali penu nyinyi na wale mliowafanya washirika wa Mungu." Kisha tutawatenga baina yao. Na hao waliowashirikisha watasema: "Nyinyi hamkuwa mkituabudu sisi."

فَكَفَىٰ بِاللَّهِ شَهِيدًا بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ إِن كُنَّا عَنْ عِبَادَتِكُمْ لَغَافِلِينَ ﴿٢٩﴾

29. "Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi baina yetu na baina yenu. Hakika sisi tulikuwa hatuna habari ya ibada yenu. (Sisi tulikuwa masanamu, hatuoni hatusikii, hatuna habari kuwa tunaabudiwa)."

هُنَالِكَ تَبْلُو كُلُّ نَفْسٍ مَّا أَسْلَفَتْ ۚ وَرُدُّوا إِلَى اللَّهِ مَوْلَاهُمُ الْحَقِّ ۖ وَضَلَّ عَنْهُم مَّا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿٣٠﴾

30. Huko kila mtu atayajua aliyoyatanguliza. Na watarudishwa kwa Mwenyezi Mungu, Mola wao wa haki. Na yatawapotea yale waliyokuwa wakiyazua.

قُلْ مَن يَرْزُقُكُم مِّنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ أَمَّن يَمْلِكُ السَّمْعَ وَالْأَبْصَارَ وَمَن يُخْرِجُ الْحَيَّ مِنَ الْمَيِّتِ وَيُخْرِجُ الْمَيِّتَ مِنَ الْحَيِّ وَمَن يُدَبِّرُ الْأَمْرَ ۚ فَسَيَقُولُونَ اللَّهُ ۚ فَقُلْ أَفَلَا تَتَّقُونَ ﴿٣١﴾

31. Sema: "Ni nani anayekuruzukuni kutoka mbinguni (kwa kuleta mvua) na katika ardhi (kwa kuotesha mimea)? Au ni nani anayemiliki masikio (yenu) na macho (yenu)? Na nani amtoaye mzima katika mfu na kumtoa mfu katika mzima? Na nani atengezaye mambo yote?" Watasema: "Ni Mwenyezi Mungu." Basi sema: "Je! Hamuogopi? (Mnawaabudu wengine pamoja naye)!"

فَذَٰلِكُمُ اللَّهُ رَبُّكُمُ الْحَقُّ ۖ فَمَاذَا بَعْدَ الْحَقِّ إِلَّا الضَّلَالُ ۖ فَأَنَّىٰ تُصْرَفُونَ ﴿٣٢﴾

32. Basi huyo ndiye Mwenyezi Mungu, Mola wenu wa haki. Na ni nini kiko baada ya (kuacha) haki, isipokuwa upotofu (upotevu)? Basi mnageuzwa wapi?

كَذَٰلِكَ حَقَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ عَلَى الَّذِينَ فَسَقُوا أَنَّهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٣٣﴾

33. Hivi ndivyo kauli ya Mola wako itakavyowathubutikia wale walioasi, ya kwamba hawataamini (kwa kuwa ni washupavu, hawataki kufuata haki).

---

26. Wametia ukafiri wao kwa ujanja hapa katika maelezo ya Aya waliyoifanya kuwa ni ya 27. Wamesema 'Neno *Ziyaadah,'* (Zaidi), linaonyesha ya kwamba: "Waaminio watampata Mungu Mwenyewe kuwa malipo yao." Nani waliyemuona amefasiri hivi katika wafasiri wote waliokuwako ulimwenguni au walioko sasa? Huu ni ukafiri wao wa kumdaia utume mtu wao na kumnasibishia Mungu Nisba mbaya baina yake na huyo mtu wao. Waliosoma vitabu vyao wameiona nisba mbaya kabisa isiyoingia akilini wanayomnasibishia Mwenyezi Mungu na huyo mtu wao. Siwezi mimi kuitaja na kuiandika hapa. Inatosha hiyo ya kudai Utume na kuwa Mwenyezi Mungu anasema naye.

34. Sema: "Je! (Yuko) katika hao mnaomshirikisha Mwenyezi Mungu, aliyeanzisha kuumba viumbe, kisha atavirejeshea?" Sema: "Mwenyezi Mungu ndiye aliyeanzisha viumbe kisha ndiye atakayevirejesha. Basi mnageuziwa wapi? (Katika upotofu (upotevu) mkaacha haki)?"

قُلْ هَلْ مِنْ شُرَكَائِكُمْ مَنْ يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ ۚ قُلِ اللَّهُ يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ ۖ فَأَنَّىٰ تُؤْفَكُونَ ﴿٣٤﴾

35. Sema "Je! Yuko katika hao mnaomshirikisha Mwenyezi Mungu aongozaye katika haki?" Sema: "Mwenyezi Mungu ndiye anayeongoza katika haki." Basi aongozaye katika haki siye anayestahiki zaidi kufuatwa au (anastahiki) yule asiyeongoka (hata yeye mwenyewe) isipokuwa aongozwe? Basi mumekuwaje? Mnahukumuje?"

قُلْ هَلْ مِنْ شُرَكَائِكُمْ مَنْ يَهْدِي إِلَى الْحَقِّ ۚ قُلِ اللَّهُ يَهْدِي لِلْحَقِّ ۗ أَفَمَنْ يَهْدِي إِلَى الْحَقِّ أَحَقُّ أَنْ يُتَّبَعَ أَمَّنْ لَا يَهِدِّي إِلَّا أَنْ يُهْدَىٰ ۖ فَمَا لَكُمْ كَيْفَ تَحْكُمُونَ ﴿٣٥﴾

36. Na wengi wao hawafuati ila dhana tu (sio ujuzi na maarifa). Na dhana haifai mbele ya haki hata kidogo. Hakika Mwenyezi Mungu anajua yote wanayoyatenda.

وَمَا يَتَّبِعُ أَكْثَرُهُمْ إِلَّا ظَنًّا ۚ إِنَّ الظَّنَّ لَا يُغْنِي مِنَ الْحَقِّ شَيْئًا ۚ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ بِمَا يَفْعَلُونَ ﴿٣٦﴾

37. Na haiwezekani kuwa hii Qurani imetungwa, haitokani na Mwenyezi Mungu (kama mnavyojidai). Bali (imetokana na Mwenyezi Mungu), inayasadikisha yaliyo mbele yake, na ni maelezo ya vitabu (vilivyopita). Haina shaka kuwa imetoka kwa Mola wa walimwengu (wote).

وَمَا كَانَ هَٰذَا الْقُرْآنُ أَنْ يُفْتَرَىٰ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَلَٰكِنْ تَصْدِيقَ الَّذِي بَيْنَ يَدَيْهِ وَتَفْصِيلَ الْكِتَابِ لَا رَيْبَ فِيهِ مِنْ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٣٧﴾

38. Je! Ndiyo wanasema ameitunga? Sema: "Hebu (tungeni na nyiye) mlete sura moja mfano wake na waiteni muwezao (kuwapata waje)—isipokuwa Mwenyezi Mungu—(wa kuwasaidieni) kama nyinyi mnasema kweli (kuwa haya ameyazua Muhammad)."

أَمْ يَقُولُونَ افْتَرَاهُ ۖ قُلْ فَأْتُوا بِسُورَةٍ مِثْلِهِ وَادْعُوا مَنِ اسْتَطَعْتُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٣٨﴾

39. Bali wameyakadhibisha wasiyoyajua hakika yake wala hakika yake haijawafikia bado uwongo wake wala ukweli wake (kwani hawakutazama hayo, ila walijikatia tu wakasema 'Uwongo'). Namna hivi walikadhibisha waliokuwa kabla yao. (Walikadhibisha bila kutazama kwanza kuwa kweli au uwongo). Basi kaangalie jinsi ulivyokuwa mwisho wa madhalimu hao.

بَلْ كَذَّبُوا بِمَا لَمْ يُحِيطُوا بِعِلْمِهِ وَلَمَّا يَأْتِهِمْ تَأْوِيلُهُ ۚ كَذَٰلِكَ كَذَّبَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ ۖ فَانْظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الظَّالِمِينَ ﴿٣٩﴾

40. Na miongoni mwao (hao Makureshi na wengineo) wako wanaoiamini, na miongoni mwao wako wasioiamini. Na Mola wako anawajua vyema waharibifu.

وَمِنْهُمْ مَنْ يُؤْمِنُ بِهِ وَمِنْهُمْ مَنْ لَا يُؤْمِنُ بِهِ ۚ وَرَبُّكَ أَعْلَمُ بِالْمُفْسِدِينَ ﴿٤٠﴾ ع

---

Na wamesema uwongo tena walipoandika: "neno *al-Husnaa* (lenye pia maana ya kumuona Mungu)." Uwongo kabisa! Hakuna mfasiri yo yote aliyefasiri *Al-Husnaa* = kumuona Mungu. Lakini yote haya ni kutaka kumthubutishia mtu wao hayo majidai yake anayojidai ya kuwa anaonana na Mungu na kuzungumza naye!

26-27. Kama ada ya Mwenyezi Mungu katika Qurani—akitaja ya wema hutaja na ya wabaya.

28-29. Namna wenye kuabudiwa watakavyowabamanduka (watakavyowatatua) waliowaabudu.

31-35. Wanasimangwa kuambiwa hao wanaowaabudu wamefanya nini. Hawana lao jambo.

41. Na kama wakiendelea kukukadhibisha sema: "Mimi nina amali yangu na nyinyi mna amali yenu. Nyinyi hamna dhima na ninayoyatenda mimi (hamtalipwa nyinyi), wala mimi sina dhima na mnayoyatenda nyinyi (sitalipwa mimi)."

وَإِن كَذَّبُوكَ فَقُل لِّي عَمَلِي وَلَكُمْ عَمَلُكُمْ ۖ
أَنتُم بَرِيئُونَ مِمَّا أَعْمَلُ وَأَنَا بَرِيءٌ مِّمَّا
تَعْمَلُونَ ﴿٤١﴾

42. Na wako miongoni mwao wanaokusikiliza (lakini si kwa haja ya kutaka kufahamu). Basi unaweza kuwasikilizisha viziwi ingawa hawataki kufahamu?

وَمِنْهُم مَّن يَسْتَمِعُونَ إِلَيْكَ ۚ أَفَأَنتَ تُسْمِعُ الصُّمَّ
وَلَوْ كَانُوا لَا يَعْقِلُونَ ﴿٤٢﴾

43. Na wako miongoni mwao wanaokukodolea macho (kukutazama kwa kejeli tu). Je! Unaweza kuwaongoza vipofu ingawa hawataki kuona?

وَمِنْهُم مَّن يَنظُرُ إِلَيْكَ ۚ أَفَأَنتَ تَهْدِي الْعُمْيَ
وَلَوْ كَانُوا لَا يُبْصِرُونَ ﴿٤٣﴾

44. Hakika Mwenyezi Mungu hawadhulumu watu chochote; lakini watu wanajidhulumu (wenyewe) nafsi zao. (Wamepewa mianga ya maarifa hawataki kutumia).

إِنَّ اللَّهَ لَا يَظْلِمُ النَّاسَ شَيْئًا وَلَٰكِنَّ النَّاسَ
أَنفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿٤٤﴾

45. Na (wakumbushe) siku atakayowakusanya; (waone) kama kwamba hawakukaa (duniani) ila saa moja tu ya mchana. (Akili zimewaruka hata hawajui kiasi cha wakati). Watajuana; (lakini kila mmoja hana haja na mwenziwe). Hakika watakhasirika wale waliokadhibisha kukutana na Mwenyezi Mungu, wala hawatakuwa wenye kuongoka.

وَيَوْمَ يَحْشُرُهُمْ كَأَن لَّمْ يَلْبَثُوا إِلَّا سَاعَةً مِّنَ
النَّهَارِ يَتَعَارَفُونَ بَيْنَهُمْ ۚ قَدْ خَسِرَ الَّذِينَ كَذَّبُوا
بِلِقَاءِ اللَّهِ وَمَا كَانُوا مُهْتَدِينَ ﴿٤٥﴾

46. Na kama tukikuonyesha (papa hapa ulimwenguni) baadhi ya yale tunayowaonya au tukikufisha (kabla yake; yote ni sawasawa, tutawaadhibu tu). Marejeo yao ni kwetu. Kisha Mwenyezi Mungu ni Shahidi juu ya (yote) wanayoyatenda.

وَإِمَّا نُرِيَنَّكَ بَعْضَ الَّذِي نَعِدُهُمْ أَوْ نَتَوَفَّيَنَّكَ
فَإِلَيْنَا مَرْجِعُهُمْ ثُمَّ اللَّهُ شَهِيدٌ عَلَىٰ مَا
يَفْعَلُونَ ﴿٤٦﴾

---

37. Wanaonyeshwa ukweli wa Qurani. Haipingani na ya kweli yaliyomo katika vitabu vya Mitume wote wa haki waliotangulia.

38. Wanatiwa MBARONI. Wanaambiwa walete walau sura moja tu inayoweza kulingana na Sura hizi 114 za Qurani. Hawakuweza kattu.

41. Kama hawataki basi "Muomba chumvi huombea chunguche." Wafanyiwe nini zaidi kuliko kubainishiwa hivi?

42-43. Kuonyesha kuwa hao hawana haja ya Haki. Haja yao ni kufuata yale waliyo nayo tu ya kuwadhulumu na kuwadhalilisha wenziwao. Kila kitu kiwe katika mikono yao tu basi.

45. Wanatajiwa baadhi ya yatakayotokea Akhera.

46. Anayakinishiwa Mtume kuwa anayoambiwa—ya kuteswa maadui zake—yatakuwa tu. Lakini Mwenyezi Mungu hana haraka. Anazidi kuwastahamilia.

Hapa katika hii Aya waliyoifanya ya 47 wameweka mtego ili wawatie humo Waislamu. Huyo mtu wao ametoa chungu ya ahadi katika vitabu vyake kuwa watakaompinga litawafika hili na hili . . . kama alivyoambiwa na mungu wake. Na hata moja halikutokea. Ndio anapachikia hapa: "bishara zenye maonyo na matishio ya kufika adhabu zinaweza kuachwa zisitimizwe." Uwongo! Aya hii sivyo inavyosema. Hii inamwambia Mtume, kuwa si lazima kuwa yeye atakuwa bado yu hai zitakapokuja jaza za ubaya wao huo. Jaza nyingine zitawafika, na Mtume yu hai, azione kwa macho yake—na nyingine zitakuja baada ya kufa kwake; siyo kama wanavyosema wao kuwa zinaweza kuwa "Zisitimizwe." Maneno ya Mungu yasitimizwe! Mwenyezi Mungu amekariri—kama katika Aya ya 122 ya *Suratun Nisaa* na Aya ya 115 ya *Suratul An-am*—kuwa "Nani Mkweli kuliko Mwenyezi Mungu" na "Yatatimia

47. Na kila umma (ulikuwa) una Mtume. Basi anapofika Mtume wao (wakamkadhibisha), huhukumiwa baina yao kwa uadilifu; nao hawadhulumiwi.

وَلِكُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولٌ ۖ فَإِذَا جَاءَ رَسُولُهُمْ قُضِيَ
بَيْنَهُم بِالْقِسْطِ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ (٤٧)

48. Na wanasema (Hawa makafiri): "Lini ahadi hii (itatokea ya kuadhibiwa) kama mnasema kweli?"

وَيَقُولُونَ مَتَىٰ هَٰذَا الْوَعْدُ إِن كُنتُمْ
صَادِقِينَ (٤٨)

49. Sema: "Similiki kwa ajili ya nafsi yangu (kujiondoshea) dhara wala (kujivutia) nafuu, (seuze kukufanyieni nyinyi). Lakini apendayo Mwenyezi Mungu (ndiyo huwa). Kila umma una muda wake. Unapofika muda wao hawakawii saa moja wala hawatangulii."

قُل لَّا أَمْلِكُ لِنَفْسِي ضَرًّا وَلَا نَفْعًا إِلَّا
مَا شَاءَ اللَّهُ ۗ لِكُلِّ أُمَّةٍ أَجَلٌ ۚ إِذَا جَاءَ أَجَلُهُمْ فَلَا
يَسْتَأْخِرُونَ سَاعَةً ۖ وَلَا يَسْتَقْدِمُونَ (٤٩)

50. Sema: "Mnaonaje kama ikikujieni hiyo adhabu Yake usiku au mchana, (mtaweza kukimbia)? Basi kwa nini wale wenye makosa wanaitaka ije kwa haraka?

قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ أَتَاكُمْ عَذَابُهُ بَيَاتًا أَوْ نَهَارًا مَّا
ذَا يَسْتَعْجِلُ مِنْهُ الْمُجْرِمُونَ (٥٠)

51. Ikishatokea ndiyo mtaiamini? (Mtaambiwa wakati huo): 'Je! Sasa (ndiyo mnaamini?) Na mlikuwa mkiihimiza?'

أَثُمَّ إِذَا مَا وَقَعَ آمَنتُم بِهِ ۚ آلْآنَ وَقَدْ كُنتُم بِهِ
تَسْتَعْجِلُونَ (٥١)

52. Kisha waliodhulumu (nafsi zao) wataambiwa, 'Ionjeni adhabu itakayokudumieni. Hamtalipwa ila kwa yale mliyokuwa mkiyachuma'.

ثُمَّ قِيلَ لِلَّذِينَ ظَلَمُوا ذُوقُوا عَذَابَ الْخُلْدِ هَلْ
تُجْزَوْنَ إِلَّا بِمَا كُنتُمْ تَكْسِبُونَ (٥٢)

53. Na wanakuuliza: Je! ni kweli hayo (unayoyasema)? Sema: "ndiyo! Naapa kwa Mola wangu, hayo ni kweli; nanyi hamuwezi kumshinda (Mwenyezi Mungu)."

وَيَسْتَنبِئُونَكَ أَحَقٌّ هُوَ ۖ قُلْ إِي وَرَبِّي إِنَّهُ
لَحَقٌّ ۖ وَمَا أَنتُم بِمُعْجِزِينَ (٥٣)

54. Na kama kila mtu aliyedhulumu angalikuwa na (yote) yaliyomo ardhini, bila shaka angeyatoa (yote kwa) kujikombolea. Na watakapoiona adhabu watajitahidi kuficha majuto (yao. Lakini wapi! Yatadhihiri wakitaka wasitake). Na kutahukumiwa baina yao kwa uadilifu. Nao hawatadhulumiwa.

وَلَوْ أَنَّ لِكُلِّ نَفْسٍ ظَلَمَتْ مَا فِي الْأَرْضِ
لَافْتَدَتْ بِهِ ۗ وَأَسَرُّوا النَّدَامَةَ لَمَّا
رَأَوُا الْعَذَابَ ۖ وَقُضِيَ بَيْنَهُم بِالْقِسْطِ ۚ وَهُمْ لَا
يُظْلَمُونَ (٥٤)

---

maneno yake kwa ukweli na uadilifu." Maneno ya Mungu yasitimie? Maneno yao ndiyo si ya kutimizika. Hayakutimia. Hayatimii wala Hayatatimia.

Waongo waongo — Hapana shaka wongo
Hakuna litalotimu — Katika wao uwongo

49. Mtume anaambiwa aseme hajimilikii kujiletea la nafuu—Mwenyezi Mungu akiwa hataki—wala hajimilikii kujiondoshea madhara. Na kuna watu wanaoitakidi kuwa hao wanaowaomba—wakiwa wahai au ni wafu—wanaweza kufanya haya. Basi huu ni mfano mmoja katika hayo mambo yao yanayoonyesha mwisho wa ujinga. Uislamu ni huu:

50. Wanaonywa wasiifanyie maskhara adhabu ya Mungu, kama vile wanavyosema "Mbona haiji? Naije tuione . . ." Wakati huo kutubia kwao hakutakubaliwa.

52. Katika Aya waliyoifanya ya 53 wamesema uwongo tena ambayo ndiyo kazi yao. Wameandika "Si muradi wake adhabu isiyo na mwisho." Wanathubutu kusema "Si . . ." na hali ya kuwa wanajua kuwa hii ndiyo tafsiri

55. Sikilizeni! Bila shaka (vyote) vilivyomo katika mbingu na ardhi ni vya Mwenyezi Mungu. Sikilizeni! Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni haki. Lakini wengi katika wao hawajui.

أَلَآ إِنَّ لِلَّهِ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضِ ۗ
أَلَآ إِنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ وَّلٰكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا
يَعْلَمُونَ ﴿٥٥﴾

56. Yeye (Mungu) ndiye anayehuisha na anayefisha. Na kwake mtarejeshwa (nyote).

هُوَ يُحْيٖ وَيُمِيتُ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٥٦﴾

57. Enyi watu! Yamekujieni mawaidha kutoka kwa Mola wenu na poza la (dawa ya) yale yaliyomo vifuani, na uwongofu (mkubwa) na rehema kwa wanaoamini. (Nayo ni Qurani ambayo ikifuatwa humtengezea mtu dunia yake na Akhera yake).

يٰٓأَيُّهَا النَّاسُ قَدْ جَآءَتْكُمْ مَّوْعِظَةٌ مِّنْ رَّبِّكُمْ
وَشِفَآءٌ لِّمَا فِي الصُّدُورِ ۙ وَهُدًى وَّرَحْمَةٌ
لِّلْمُؤْمِنِينَ ﴿٥٧﴾

58. Sema: "Kwa fadhila za Mwenyezi Mungu na kwa rehema yake (ndiyo mumepata haya)." Basi na wafurahi kwa hayo. Haya ni bora kuliko hivyo wanavyovikusanya.

قُلْ بِفَضْلِ اللَّهِ وَبِرَحْمَتِهٖ فَبِذٰلِكَ فَلْيَفْرَحُوا ۗ
هُوَ خَيْرٌ مِّمَّا يَجْمَعُونَ ﴿٥٨﴾

59. Sema: "Je! Mnaonaje zile riziki alizokuteremshieni Mwenyezi Mungu kisha mkafanya — katika hizo — (nyingine kuwa za) haramu na (nyingine kuwa za) halali." Sema: "Je! Mwenyezi Mungu amekuruhusuni (kufanya hivyo) au mnamzulia Mwenyezi Mungu uwongo tu?"

قُلْ أَرَءَيْتُمْ مَّآ أَنْزَلَ اللَّهُ لَكُمْ مِّنْ رِّزْقٍ
فَجَعَلْتُمْ مِّنْهُ حَرَامًا وَّحَلٰلًا ۗ قُلْ ءٰٓاللَّهُ
أَذِنَ لَكُمْ أَمْ عَلَى اللَّهِ تَفْتَرُونَ ﴿٥٩﴾

---

iliyofasiriwa na chungu kabisa ya wanavyuoni; na hao waliofasiri vingine ni wachache kabisa kabisa. Lakini wao wakikitaka kitu hufanya hicho tu ndicho chenye kukubaliwa, japokuwa sicho chenye kukubaliwa.

54. Wanatajiwa baadhi ya yatakayotokea Akhera. Hakuna kikomboleo huko hata mtu akiitowa dunia nzima—kama ni yake—akampa Mungu, asingepokelea; adhabu tu inamngojea.

57-59. Wanatajiwa wanaadamu fadhila kubwa kabisa iliyowajia kwa kuteremshiwa Qurani aliyokuja nayo Nabii Muhammad; tena wanatakiwa waishukuru neema hiyo—si Waislamu tu. Kwani Ustaarabu tunaouona umetapakaa ulimwengu mzima kwa wasita wa Wazungu, hawa Wazungu wameupata kwa Waislamu walipotawaliwa na hao Waislamu huko kwao Ulaya. Wakakaa chini ya utawala wa Kiislamu kwa upande wa Magharibi kiasi cha miaka mia sita, na kwa upande wa Mashariki kiasi cha miaka mia nne. Wakati huo ndipo walipouona ustaarabu wa Kiislamu na wakasoma ilimu za Kiislamu katika Ma-University makubwa ya Kiislamu. Mpaka baadhi ya Ma-Pope walisoma katika maskuli hayo ya Waislamu yaliyokuwako huko Ulaya na yaliyokuwako Asia nzima na yaliyokuwako Kaskazini ya Africa. Kama sasa watu wanavyokwenda kusoma katika maskuli ya Wazungu, basi ndivyo ilivyokuwa hapo zamani—hata wasiokuwa Waislamu—wanakwenda kusoma katika Skuli za Kiislamu. Basi hii wanayoitapakaza sasa ulimwenguni ni bidhaa waliyoipata kwa Waislamu; wakakisia kwa hiyo, wakaongezea

Kama si wenyewe Tungeyasemaje

Basi—kama wanajua fadhila—nawaushukuru Uislamu na Mtume wake—Nabii Muhammad—badala ya kumtaja kwa uovu wa kumsingizia tu.

59. Maqureshi walikuwa na wanyama na vyakula walivyokuwa wakisema kuwa ni Haramu kuliwa—navyo si haramu—na vyengine kuwa ni Halali—navyo si halali. Miongoni mwa wanyama waliokuwa wakisema Haramu kuliwa kama ilivyo katika Aya ya 103 ya *Surat Maida*:—

(a) Ngamia jike aliyezaa mimba 10.

60. Na ni nini dhana ya wale wanaomzulia Mwenyezi Mungu uwongo, juu ya siku ya Kiyama? Hakika Mwenyezi Mungu ana fadhila (wema) nyingi juu ya watu. Lakini wengi wao hawashukuru.

وَمَا ظَنُّ الَّذِينَ يَفْتَرُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَذُو فَضْلٍ عَلَى النَّاسِ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَشْكُرُونَ ﴿٦٠﴾

61. Na hushughuliki katika kazi yoyote, wala husomi humo (kitu chochote) katika Qurani wala hamfanyi kitendo chochote (chengine), isipokuwa Sisi tunakuwa mashahidi juu yenu mnaposhughulika nayo. Hakifichikani kwa Mola wako kitu chochote (hata) kilicho sawa na uzito wa mdudu chungu, la katika ardhi wala katika mbingu. Wala (hapana) kidogo kuliko hicho wala kikubwa, isipokuwa kimo katika Kitabu (cha Mwenyezi Mungu) kielezacho (kila kitu).

وَمَا تَكُونُ فِي شَأْنٍ وَمَا تَتْلُو مِنْهُ مِنْ قُرْآنٍ وَلَا تَعْمَلُونَ مِنْ عَمَلٍ إِلَّا كُنَّا عَلَيْكُمْ شُهُودًا إِذْ تُفِيضُونَ فِيهِ ۚ وَمَا يَعْزُبُ عَنْ رَبِّكَ مِنْ مِثْقَالِ ذَرَّةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي السَّمَاءِ وَلَا أَصْغَرَ مِنْ ذَٰلِكَ وَلَا أَكْبَرَ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُبِينٍ ﴿٦١﴾

62. Sikilizeni! Vipenzi vya Mwenyezi Mungu hawatakuwa na khofu (siku ya Kiyama) wala hawatahuzunika.

أَلَا إِنَّ أَوْلِيَاءَ اللَّهِ لَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٦٢﴾

63. Nao ni wale walioamini na wakawa wanamcha Mungu (wanafuata amri Zake na wanajiepusha na makatazo yake).

الَّذِينَ آمَنُوا وَكَانُوا يَتَّقُونَ ﴿٦٣﴾

64. Wao wana mema katika maisha ya duniani na katika Akhera. Hakuna mabadiliko katika maneno ya Mwenyezi Mungu. Huku ndiko kufuzu kukubwa.

لَهُمُ الْبُشْرَىٰ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ ۚ لَا تَبْدِيلَ لِكَلِمَاتِ اللَّهِ ۚ ذَٰلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿٦٤﴾

---

(b) Kondoo jike au mbuzi aliyezaa mimba 5.

(c) Dume—wa ngamia au mbuzi au kondoo au ng'ombe—aliyezaliwa pacha na jike.

(d) Beberu lililozalisha majike wengi hapo kwao na mtaani. Likiwa dume hilo la ngamia au ng'ombe au kondoo au mbuzi.

Na katika wanyama waliokuwa wakisema Halali kuliwa kama ilivyo katika Aya ya 139 ya *Suratil An-Am* ni mizoga (iliyokufa wenyewe bila ya kuchinjwa).

Na kuharamisha kwao baadhi ya vyakula ambavyo si haramu kumetajwa katika Aya ya 138 ya *Suratil An-Am.*

61. Aya hii inaonyesha kuwa Mwenyezi Mungu halimfichikii lolote; analijua kila jambo lililopita na lililoko na linalokuja . . . Na Aya hii inaonyesha kuwa katika mambo yetu na mikutano yetu zitolewe stishhadi za Qurani, watu wasikie ya Mungu. Na kama hawajui maana yake wafasiriwe.

Lakini yako wapi haya sasa kwetu sisi. Sasa makasida tu yasiyofasiriwa. Na bora yasifasiriwe, kwani mengine yanaonyesha ukafiri dhahiri kama ile kasida inayosema:—

Waniimal Waali Waaliyha

Na nyingine zinazoonyesha kuvunja hishima za Mitume kama tulivyobainisha katika Aya ya 253 ya *Suratul Baqarah* iliyo katika Juzuu ya tatu.

63. Hapa Mwenyezi Mungu anawataja mawilii na sifa zao. Nao ni kuwa wanamuogopa Mwenyezi Mungu—wanafanya aliyowaamrisha na wanajiepusha na aliyowakataza.

Hawakuambiwa wana Siwa wala Matuwazi wala . . . wala kuwa wao ni watu makhsusi—Masharifu na Mashekhe hao tu basi.

Uwongo kabisa habari hiyo. Yaliyo kweli ni haya:— Kila anayefuata yaliyo katika hii Aya ya 63 ndiye Walii: Wewe au Yeye au Mimi pia, hata ikiwa hatupigiwi Mbiu ya Mgambo ambayo Ikilia ina Jambo.

Hizo zilizosalia ni propaganda za kudanganyia watu.

65. Wala (Wewe Mtume—na wengineo pia) yasikuhuzunishe maneno yao (wanayokukutukanieni). Hakika utukufu wote ni wa Mwenyezi Mungu. Yeye ndiye asikiaye na ajuaye.

وَلَا يَحْزُنكَ قَوْلُهُمْ ۘ إِنَّ الْعِزَّةَ لِلَّهِ
جَمِيعًا ۚ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٦٥﴾

66. Sikilizeni! Bila shaka (vyote) vilivyomo katika mbingu na vilivyomo katika ardhi ni vya Mwenyezi Mungu. Na wale wanaoabudu wasiokuwa Mwenyezi Mungu, hawafuati washirika (wa Mwenyezi Mungu, kwani Mungu hana washirika); hawafuati ila dhana tu. Nao hawasemi ila uwongo tu.

أَلَا إِنَّ لِلَّهِ مَن فِي السَّمَاوَاتِ وَمَن فِي الْأَرْضِ ۗ
وَمَا يَتَّبِعُ الَّذِينَ يَدْعُونَ مِن دُونِ اللَّهِ
شُرَكَاءَ ۚ إِن يَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ وَإِنْ هُمْ إِلَّا
يَخْرُصُونَ ﴿٦٦﴾

67. Yeye (Mwenyezi Mungu) ndiye aliyekufanyieni usiku ili humo mtulie, na (akakufanyieni) mchana ung'arao (ili muonee). Hakika katika hayo zimo ishara (za kuonyesha neema za Mwenyezi Mungu juu ya viumbe vyake) kwa watu wanaosikia.

هُوَ الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ اللَّيْلَ لِتَسْكُنُوا فِيهِ
وَالنَّهَارَ مُبْصِرًا ۚ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ
لِّقَوْمٍ يَسْمَعُونَ ﴿٦٧﴾

68. Wanasema: "Mwenyezi Mungu amejifanyia mtoto." Ameepukana na hayo. Yeye anajitosheleza (hahitajii mtoto wala mshirika wala yoyote yule). Ni vyake (peke yake vyote) vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini. Nyinyi hamna dalili kwa hayo (ya uwongo mnayoyasema). Je! Mnajisemea tu juu ya Mwenyezi Mungu msiyoyajua?

قَالُوا اتَّخَذَ اللَّهُ وَلَدًا ۗ سُبْحَانَهُ ۖ هُوَ الْغَنِيُّ ۖ لَهُ مَا
فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۚ إِنْ عِندَكُم مِّن
سُلْطَانٍ بِهَٰذَا ۚ أَتَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ مَا لَا
تَعْلَمُونَ ﴿٦٨﴾

69. Sema: "Wale wanaomzulia Mwenyezi Mungu uwongo hawatafaulu."

قُلْ إِنَّ الَّذِينَ يَفْتَرُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ
لَا يُفْلِحُونَ ﴿٦٩﴾

70. Ni starehe chache tu katika dunia, kisha kwetu ndiyo marejeo yao. Hapo tutawaonjesha adhabu kali kwa sababu ya kule kukufuru kwao.

مَتَاعٌ فِي الدُّنْيَا ثُمَّ إِلَيْنَا مَرْجِعُهُمْ ثُمَّ نُذِيقُهُمُ
الْعَذَابَ الشَّدِيدَ بِمَا كَانُوا يَكْفُرُونَ ﴿٧٠﴾

Basi kwa kufanya hivyo mtu huhisabika kipenzi cha Mwenyezi Mungu, (Walii). Siyo kuwa kuna watu makhsusi wanaovaa kivazi makhsusi au wenye kabila makhsusi au wanaokaa mahala makhsusi; hao ndio wanaoitwa mawalii. Huu uzushi tu na udanganyaji. Hakuna anayijua tafsiri ya tamko la Walii kuliko Mwenyewe Mwenyezi Mungu; naye amekwisha kulifasiri hivi. Basi tusizue yasiyokuwako.

64. Haya ndiyo yatakayowathubutikia Mawalii siyo kuleta Makarama. Hayo Makarama anapotaka Mwenyewe Mwenyezi Mungu huwapa, siyo wenyewe wanayaleta saa watakayo au dakika na nyakati wapendazo. Hayo yanayofanywa kwa saa na dakika na yakati ni uchawi tu na viini macho vya hao wanaojinasibishia Uwalii. Na mengi kabisa ni hadithi za uwongo tu. Hayakutokea kattu. Wanayabuni wenyewe na VIBARAKA wao—wakayatapakaza kila mahala.

Na huko kusema kwao kuwa Bwana Fulani aliposikia kuwa mtu fulani anayemkusudia—au anayekusudia shughuli yake—amezama, alisema "Kama kweli amenikusudia mimi hatakufa maji ataokoka tu, ila ikiwa muongo katika mapenzi yake ndiyo atazama; akaokoka, akatoka salama yeye tu—roho tupu na kiwiliwili chake kitupu, uchi hana hata kitema." Wambie watu hao kwa kinywa kipana "Kwa nini basi huyo aliyemkusudia yeye tu, ndiye aliyefikwa na maafa hayo—ya kuzama akapoteza kila chake, hata hizo zawadi alizoazimu kumletea?"

Haya ni kama majidai ya Mayahudi na Manasra na jawabu aliyowajibu Mwenyezi Mungu, kama ilivyo katika Aya ya 20 ya *Suratul Maida* Juzuu ya 6.

Katika maelezo ya Aya hii waliyoifanya ya 65 wametia ukafiri wao ule mkubwa wa kumdai Utume mtu wao, wakasema: "Neno *Bushraa* (habari njema) lina matumizi mapana na linaweza kutumiwa kwa kuhusu wahyi na njozi za Manabii, pia za mawalii na waaminio; na Aya hii inahusu namna zote hizi mbili za njozi na wahyi (Jarir na Kathir)." Wallahi! Hamna humo katika tafsiri ya Ibni Jarir na Ibni Kathir kusema: "Wahyi wa mawalii na waaminio." Wamekuwa Pweza—wanajipalia wenyewe makaa ya Moto wa Jahanamu. Hawakusikia nadhani:

71. Wasomee khabari za Nuhu alipowaambia watu wake: "Enyi watu wangu! Ikiwa kukaa kwangu na nyinyi na kukumbusha kwangu Aya za Mwenyezi Mungu kunakuchukizeni, basi mimi nategemea kwa Mwenyezi Mungu. Nanyi kusanyeni mambo yenu na hao washirika wenu. (Kusanyikeni mje kunidhuru; mimi sijali). Tena shauri lenu hilo lisifichikane kwenu (fanyeni kwa dhahiri; mimi sijali tu). Kisha mpitishe kwangu (hilo mnalotaka kulipitisha). Wala msinipe nafasi (hata kidogo. Mimi sijali, namtegemea Mwenyezi Mungu tu).

وَاتْلُ عَلَيْهِمْ نَبَأَ نُوحٍ ۘ إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِ يَٰقَوْمِ إِن كَانَ كَبُرَ عَلَيْكُم مَّقَامِي وَتَذْكِيرِي بِـَٔايَٰتِ اللَّهِ فَعَلَى اللَّهِ تَوَكَّلْتُ فَأَجْمِعُوٓا أَمْرَكُمْ وَشُرَكَآءَكُمْ ثُمَّ لَا يَكُنْ أَمْرُكُمْ عَلَيْكُمْ غُمَّةً ثُمَّ اقْضُوٓا إِلَيَّ وَلَا تُنظِرُونِ ﴿٧١﴾

72. Lakini mkikengeuka (khiari yenu). Mimi sikuombeni ujira (sini)! Ujira wangu hauko ila kwa Mwenyezi Mungu. Na nimeamrishwa niwe miongoni mwa wanaojisalimisha kwake (wakamtegemea yeye; basi nimemtegemea yeye, sijali kitu)."

فَإِن تَوَلَّيْتُمْ فَمَا سَأَلْتُكُم مِّنْ أَجْرٍ ۖ إِنْ أَجْرِيَ إِلَّا عَلَى اللَّهِ ۖ وَأُمِرْتُ أَنْ أَكُونَ مِنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿٧٢﴾

73. Lakini walimkadhibisha. Basi tukamuokoa yeye na waliokuwa naye, katika jahazi. Na tukawafanya wao ndio waliobakia (ulimwenguni baada ya kuangamizwa hao). Na tukawazamisha wale waliozikadhibisha Aya zetu. Basi angalia jinsi ulivyokuwa mwisho wa wale walioonywa (wasisikie).

فَكَذَّبُوهُ فَنَجَّيْنَٰهُ وَمَن مَّعَهُ فِي الْفُلْكِ وَجَعَلْنَٰهُمْ خَلَٰٓئِفَ وَأَغْرَقْنَا الَّذِينَ كَذَّبُوا بِـَٔايَٰتِنَا ۖ فَانظُرْ كَيْفَ كَانَ عَٰقِبَةُ الْمُنذَرِينَ ﴿٧٣﴾

74. Kisha tukawapeleka Mitume (wengi) baada yake, kwa watu wao. Nao wakawajia kwa hoja waziwazi. Lakini hawakuwa wenye kuamini waliyoyakadhibisha zamani; (walishika yale yale waliyoyaona kwa wazee wao, wakakataa kuwafuata Mitume). Namna hivi tunapiga muhuri juu ya nyoyo za watu wanaopita mipaka.

ثُمَّ بَعَثْنَا مِنۢ بَعْدِهِ رُسُلًا إِلَىٰ قَوْمِهِمْ فَجَآءُوهُم بِالْبَيِّنَٰتِ فَمَا كَانُوا لِيُؤْمِنُوا بِمَا كَذَّبُوا بِهِ مِن قَبْلُ ۚ كَذَٰلِكَ نَطْبَعُ عَلَىٰ قُلُوبِ الْمُعْتَدِينَ ﴿٧٤﴾

75. Kisha baada ya hao tukamtuma Musa na Haruni kwa Firauni na watu wake wakubwa, kwa hoja zetu. Lakini walijivuna, wakawa watu maasi.

ثُمَّ بَعَثْنَا مِنۢ بَعْدِهِم مُّوسَىٰ وَهَٰرُونَ إِلَىٰ فِرْعَوْنَ وَمَلَإِيْهِۦ بِـَٔايَٰتِنَا فَاسْتَكْبَرُوا وَكَانُوا قَوْمًا مُّجْرِمِينَ ﴿٧٥﴾

---

| | |
|---|---|
| Salil Jahimu | Mambo mazito |
| Siyahi na zite | Katika Moto |
| Sura uwakao | Kwa mivukuto |
| Na kwenda miteo | Na kugoroma |
| Dhamirini mwako | Usisahau |
| Dhiki za Motoni | Ukadharau |
| Dhurubu mithali | Kama hiyau |
| Wadhurubiyeo | Wote ulama |

67. Mwenyezi Mungu anawatajia fadhila zake kwa kuleta mchana na usiku.

68. Wanasimangwa na kutolewa akilini kuwa wanafuata yasiyokuwa na hoja wala dalili.

71. Sasa yanatajwa baadhi ya yaliyowafika baadhi ya Mitume ili kumliwaza Mtume asione kuwa hayo yanamfika yeye tu. Akiona na wenzake yaliwafika ataliwazika kidogo, kwani kufa kwa wengi arusi.

73. Tutaona *Inshaalah* katika Sura ijayo, *Surat Hud,* namna Nabii Nuhu alivyoingia Jahazini pamoja na watoto wake watatu waliokuwa Waislamu na pamoja na watu waliomuamini; wakasalimika na tufani hiyo

76. Basi ilipowajia haki kutoka kwetu walisema: "Bila shaka huu ni uchawi dhahiri."

فلما جاءهم الحق من عندنا قالوا إن هذا
لسحر مبين ﴿٧٦﴾

77. Akasema Musa: "Mnasema (hivi) juu ya haki ilipokujieni? Huu ni uchawi? (Mbona umefaulu basi) Na wachawi hawafaulu?"

قال موسى أتقولون للحق لما جاءكم أسحر
هذا ولا يفلح الساحرون ﴿٧٧﴾

78. Wakasema: "Je! Umetujia ili utuondoe katika yale tuliyowakuta nayo baba zetu, na ili ukubwa uwe wenu nyinyi (wawili) katika nchi (hii)? Sisi hatuwezi kukuaminini."

قالوا أجئتنا لتلفتنا عما وجدنا عليه
آباءنا وتكون لكما الكبرياء في الأرض وما
نحن لكما بمؤمنين ﴿٧٨﴾

79. Na Firauni akasema: "Nileteeni kila mchawi hodari."

وقال فرعون ائتوني بكل سحر عليم ﴿٧٩﴾

80. Basi walipokuja wachawi, Musa aliwaambia: "Tupeni mnavyotaka kuvitupa (ili kuonyesha watu uhodari wenu)."

فلما جاء السحرة قال لهم موسى ألقوا ما
أنتم ملقون ﴿٨٠﴾

81. Walipotupa, Musa alisema: "Mliyoleta ni uchawi; Mwenyezi Mungu sasa hivi ataubatilisha. Hakika Mwenyezi Mungu hastawishi vitendo vya waharibifu."

فلما ألقوا قال موسى ما جئتم به السحر
إن الله سيبطله إن الله لا يصلح عمل
المفسدين ﴿٨١﴾

82. "Na Mwenyezi Mungu ataithubutisha haki kwa maneno Yake, ingawa watachukia (hao) wabaya."

ويحق الله الحق بكلماته ولو كره المجرمون ﴿٨٢﴾

83. Hawakumuamini Musa isipokuwa baadhi ya vijana vya kaumu yake (Firâuni; Ama Mayahudi walimwamini kwa kuona ni mwokozi wa kabila lao ) kwa sababu ya kumuogopa Firauni na wakuu wao, ili asiwatese. Na hakika Firauni alikuwa jeuri katika

فما آمن لموسى إلا ذرية من قومه على خوف
من فرعون وملإيهم أن يفتنهم وإن فرعون

---

(mgharikisho huo) iliyogharikisha kila kilichokuwako ulimwenguni — ulimwengu wa wakati huo.

Baada ya kumalizika taathira ya tufani hiyo ndipo walipoteremka na Nabii Nuhu wakaanza kukaa tena katika ardhi na wakaanza kuzaa—hawakuzaa mule jahazini. Basi binadamu walioko ulimwengu mzima sasa wote wanatokana na chembe mbili tatu hizo zilizokuwa mule jahazini zikasalimika na kugharikika. Bali hakika walimwengu wote walioko ulimwenguni wanatokana na wale watoto watatu tu wa Nabii Nuhu kama alivyosema Mwenyezi Mungu katika Aya 77 Sura ya *As-Saaffat*—Na akasema pia haya Mwenyezi Mungu katika Aya ya 3 ya *Surat Bani Israil.* "Enyi kizazi cha wale tuliowapandisha (katika jahazi) pamoja na Nuhu!" "Na tuliwajaalia kizazi chake wawe ndio wenye kubaki (mpaka leo ulimwenguni)."

76. Walipoona hawana la kusema kwa ile haki waliyoiona ndipo waliposukuma wakasema "Uchawi. Kiini Macho."

Katika mwisho wa maelezo ya Aya waliyoifanya kuwa ni ya 77 wametia tena ukafiri wao wa kumdaia mtu wao Utume na Unabii Isa na . . . Tumevunja ukafiri huu katika maelezo ya Aya ya 7 ya *Suratul Faatiha* na Aya ya 4 na ya 115 za *Suratul Baqarah.* Kudai Utume baada ya Nabii Muhammad ni ukafiri tu kwa madhehebu zote za Uislamu.

77. Na kama tunavyowaona wachawi na waganga. Juu ya dhambi wanazopata hawatengenekewi na yao. Na hao wanaowategemea wachawi na waganga ndio vivi hivi.

78. Lile walilonalo wao ndio wanawasingizia wenziwao. Wao ndio wanaoung'ang'ania ukubwa ili waendelee kuwadhili tu hao wanaowadhili. Wanasema kuwa Nabii Musa na ndugu yake wanatafuta ukubwa kwa hayo ya haki wanayoyasema.

81. Imebainishwa katika Aya nyingi namna Nabii Musa alivyobatilisha uchawi wao huo. Kila Mtume hupewa miujiza kwa yale waliyobobea nayo watu wa zama zake. Katika zama za Nabii Musa yalishika nguvu sana mambo

nchi. Na kwa yakini yeye alikuwa miongoni mwa (maasi) waliopita kiasi.

لَعَالٍ فِي الْأَرْضِ وَإِنَّهُ لَمِنَ الْمُسْرِفِينَ ﴿٨٣﴾

84. Na Musa akasema: "Enyi kaumu yangu! Ikiwa nyinyi mumemwamini Mwenyezi Mungu, basi mtegemeeni Yeye kama nyinyi ni Waislamu kweli."

وَقَالَ مُوسَىٰ يَا قَوْمِ إِن كُنتُمْ آمَنتُم بِاللَّهِ فَعَلَيْهِ
تَوَكَّلُوا إِن كُنتُم مُّسْلِمِينَ ﴿٨٤﴾

85. Wakasema: "Tunamtegemea Mwenyezi Mungu. Ee Mola wetu! Usitufanye wenye kutiwa misukosuko na hao watu madhalimu."

فَقَالُوا عَلَى اللَّهِ تَوَكَّلْنَا رَبَّنَا لَا تَجْعَلْنَا فِتْنَةً
لِّلْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿٨٥﴾

86. "Na utuokoe kwa rehema Yako na hao watu makafiri."

وَنَجِّنَا بِرَحْمَتِكَ مِنَ الْقَوْمِ الْكَافِرِينَ ﴿٨٦﴾

87. Na tukampelekea Wahyi Musa na ndugu yake kwa "Watengenezeeni majumba watu wenu katika mji na zifanyeni nyumba zenu ndiyo misikiti (yenu maadamu hamtathubutu kufanya ibada misikitini) na simamisheni Sala. Na uwape habari njema wanaoamini (kuwa watatengenekewa karibuni papa hapa duniani na kesho Akhera)."

وَأَوْحَيْنَا إِلَىٰ مُوسَىٰ وَأَخِيهِ أَن تَبَوَّآ
لِقَوْمِكُمَا بِمِصْرَ بُيُوتًا وَاجْعَلُوا بُيُوتَكُمْ
قِبْلَةً وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَبَشِّرِ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٨٧﴾

88. Na Musa akasema: "Mola wetu! Wewe umempa Firauni na watu wake wakubwa mapambo na mali (nyingi) katika maisha ya dunia. Mola wetu! Hivyo wanapoteza watu katika njia yako. Mola wetu! Ziangamize mali zao na uzishambulie nyoyo zao, maana hawataamini mpaka waione adhabu inayoumiza."

وَقَالَ مُوسَىٰ رَبَّنَا إِنَّكَ آتَيْتَ فِرْعَوْنَ
وَمَلَأَهُ زِينَةً وَأَمْوَالًا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا
رَبَّنَا لِيُضِلُّوا عَن سَبِيلِكَ رَبَّنَا اطْمِسْ عَلَىٰ
أَمْوَالِهِمْ وَاشْدُدْ عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ فَلَا يُؤْمِنُوا
حَتَّىٰ يَرَوُا الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿٨٨﴾

89. (Mwenyezi Mungu) akasema: "Maombi yenu yamekubaliwa. Basi tengeneeni vizuri, wala msifuate njia za wale wasiojua (wakataka wapate mambo yao mara moja)."

قَالَ قَدْ أُجِيبَت دَّعْوَتُكُمَا فَاسْتَقِيمَا وَلَا
تَتَّبِعَانِّ سَبِيلَ الَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٨٩﴾

---

ya uchawi. Basi muujiza wa Nabii Musa ulikuwa kuubatilisha kila uchawi wanaoufanya — kuupindua chini juu. Zama za Nabii Daudi zilikuwa zama ambazo chuma kinaanza kutumiwa kwa nguvu kwa kufanya silaha. Mwenyezi Mungu akamdhalilishia chuma akafanya silaha kwa namna atakayo. Zama za Nabii Isa ulikithiri udaktari. Akapewa muujiza wa kuponesha magonjwa wasiyoweza kuyaponesha. Na akapewa muujiza wa kufufua kilichokufa bali na kukipa roho kilichokuwa hakina roho.

83. Mara nyingi Mwenyezi Mungu kabainisha kuwa wanaoanza kuwafuata Mitume ni vijana si ile mizee kwani ile mizee huwa imebobea katika ubaya wao; wanaona taabu kuukosa huo ukubwa wao na hayo waliyoyazoelea, japo mabaya; kwani 'Mzoea ya kunyonga ya kuchinja haiwezi' Yanabainishwa haya hapo katika Aya ya 10, na 13, za *Suratul Kahf*.

84-86. Tumebainisha mara nyingi namna Mwenyezi Mungu anavyoamrisha tujiweke tayari kuwakabili makafiri, kisha tumtegemee yeye. Basi mambo yatanyoka.

87. Lisilomkinika kufanyika kwa ukamilifu lisiachwe kabisa kabisa. Nalifanywe japo kwa upungufu wake. Bora kidogo kuliko hapana kabisa. Ilivyokuwa hawawezi kujenga misikiti wakasali humo, wanaambiwa wasali mumo humo majumbani mwao; wafanye humo mahala pa kusalia. Tunambiwa kusali kwa kusimama. Ikitomkinika sali kwa kukaa. Ikitomkinika sali kwa kulalia ubavu wa kulia. Ikitomkinika sali kwa wa kushoto. Ikitomkinika sali kwa kulala chali. Na kama huwezi kutaharaki ashiria kwa macho — kujifahamisha kuwa sasa ndio rukuu, sasa ndio itidali, sasa . . . mpaka mwisho.

88-89. Nabii Musa anaona neema kubwa kabisa aliyo nayo Firauni na watu wake ndiyo inayowapandisha Vichwa, basi anamuomba Mwenyezi Mungu awaondolee neema hiyo; washituke kidogo warejee kwake.

90. Na tukawapitisha wana wa Israili katika bahari; na Firauni na majeshi yake wakawafuata kwa dhulma na ujeuri. Hata kulipomfikia Firauni kuzama alisema: "Naamini ya kwamba hakuna aabudiwaye kwa haki ila Yule wanayemuamini wana wa Israili, na mimi ni miongoni mwa wanaotii (kama wanavyotii wao)."

وَجٰوَزْنَا بِبَنِيٓ إِسْرَآءِيلَ الْبَحْرَ فَأَتْبَعَهُمْ
فِرْعَوْنُ وَجُنُودُهُ بَغْيًا وَعَدْوًا ۖ حَتّٰىٓ إِذَآ أَدْرَكَهُ
الْغَرَقُ قَالَ ءَامَنتُ أَنَّهُ لَآ إِلٰهَ إِلَّا الَّذِيٓ ءَامَنَتْ
بِهِ بَنُوٓا إِسْرَآءِيلَ وَأَنَا مِنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿٩٠﴾

91. (Malaika wakamwambia): "Sasa (ndiyo unaamini hayo)! Hali uliasi (muda mrefu) kabla ya hapo na ukawa miongoni mwa waharibifu."

ءَآلْـٰٔنَ وَقَدْ عَصَيْتَ قَبْلُ وَكُنتَ مِنَ
الْمُفْسِدِينَ ﴿٩١﴾

92. "Basi leo tutakuokoa kwa (kuuweka) muili wako, ili uwe dalili kwa ajili ya wa nyuma yako (wajue yakuwa hukuwa Mungu)." Na watu wengi wameghafilika na ishara zetu.

فَالْيَوْمَ نُنَجِّيكَ بِبَدَنِكَ لِتَكُونَ لِمَنْ خَلْفَكَ
ءَايَةً ۚ وَإِنَّ كَثِيرًا مِّنَ النَّاسِ عَنْ ءَايٰتِنَا
لَغٰفِلُونَ ﴿٩٢﴾

93. Na (baadaye) tuliwaweka wana Israili makazi mazuri, na tukawaruzuku vitu vizuri. Nao hawakukhitalifiana mpaka ilipowajia ilimu. Hakika Mola wako atahukumu baina yao siku ya Kiama katika yale waliyokuwa wakikhitalifiana.

وَلَقَدْ بَوَّأْنَا بَنِيٓ إِسْرَآءِيلَ مُبَوَّأَ صِدْقٍ
وَرَزَقْنٰهُم مِّنَ الطَّيِّبٰتِ فَمَا اخْتَلَفُوا
حَتّٰى جَآءَهُمُ الْعِلْمُ ۚ إِنَّ رَبَّكَ يَقْضِي بَيْنَهُمْ
يَوْمَ الْقِيٰمَةِ فِيمَا كَانُوا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ﴿٩٣﴾

94. Na kama unayo shaka juu ya hayo tuliyokuteremshia, basi waulize wale wasomao vitabu kabla yako (Mayahudi na Manasara wale waliosilimu). Kwa yakini haki imekwisha kukujia kutoka kwa Mola wako, kwa hivyo usiwe miongoni mwa wanofanya shaka

فَإِن كُنتَ فِي شَكٍّ مِّمَّآ أَنزَلْنَآ إِلَيْكَ فَسْـَٔلِ الَّذِينَ
يَقْرَءُونَ الْكِتٰبَ مِن قَبْلِكَ ۚ لَقَدْ جَآءَكَ الْحَقُّ
مِن رَّبِّكَ فَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْمُمْتَرِينَ ﴿٩٤﴾

95. Wala usiwe miongoni mwa wale wanaozikadhibisha ishara za Mwenyezi Mungu. Usije ukawa miongoni mwa wenye khasara.

وَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الَّذِينَ كَذَّبُوا بِـَٔايٰتِ اللَّهِ
فَتَكُونَ مِنَ الْخٰسِرِينَ ﴿٩٥﴾

---

Wakaambiwa watajibiwa, lakini si kwa haraka. Mwenyezi Mungu mambo yake ni taratibu.

Na sisi ndiyo vivi hivi. Tukiona hatujibiwi upesi dua zetu tusikate tamaa; atatujibu *Inshallah* utakapofika wakati wake, wakati ambao hapo ndiyo maslaha kwetu kujibiwa. Useme

Sikuayisi tamaa — Kufanikiwa muradi
Nangojea yangu saa — Saa ya sada na sudi

90-91. Mwenyezi Mungu amebainisha dhahiri—hasa katika Aya ya 18 ya *Suratun Nisaa* kuwa toba haikubaliwi wakati mauti yamekwishafika. Na mauti mtu hajui yatamshambulia lini:

Mauti sidhani — Yana muhala
Milele ziumbe — Hufa ghafula
Muamini hamba — Chenda kulala
Sipambaukiwi — Nili mzima

Basi tujitahidi kuchuma mazuri upesi na kuepuka kila mabaya

Nawe siliwaye — Ukaikuwa
Ni haki mauti — Yafaridhiwa
Numanuma taa — Ukikutiwa
Ufiye dinini — Mwake Hashima

96. Hakika wale ambao neno la Mola wako limekwishathubutika juu yao, hawataamini

إِنَّ الَّذِينَ حَقَّتْ عَلَيْهِمْ كَلِمَتُ رَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٩٦﴾

97. Ijapokuwa kila ishara itawajia; mpaka waone adhabu inayoumiza.

وَلَوْ جَآءَتْهُمْ كُلُّ ءَايَةٍ حَتَّىٰ يَرَوُا الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿٩٧﴾

98. Kwa nini usiweko mji ulioamini (upesi kabla ya kuadhibiwa), ili imani yake iwafae? Isipokuwa watu wa Yunusi (tu ndio walioamini mara walipohisi kuwa adhabu inakuja. Basi wakaokoka). Walipoamini tuliwaondolea adhabu ya hizya katika maisha ya dunia na tukawastarehesha kwa muda (tulioutaka).

فَلَوْلَا كَانَتْ قَرْيَةٌ ءَامَنَتْ فَنَفَعَهَآ إِيمَانُهَآ إِلَّا قَوْمَ يُونُسَ لَمَّآ ءَامَنُوا كَشَفْنَا عَنْهُمْ عَذَابَ الْخِزْيِ فِي الْحَيَوٰةِ الدُّنْيَا وَمَتَّعْنَٰهُمْ إِلَىٰ حِينٍ ﴿٩٨﴾

99. Na kama angalitaka Mola wako (kuwalazimisha kwa nguvu kuamini) bila shaka wangaliamini wote waliomo katika ardhi (asibaki hata mmoja). (Lakini Mwenyezi Mungu hataki kuwalazimisha watu kwa nguvu) Basi je, wewe utawashurutisha (utawashurutiza) watu kwa nguvu hata wawe Waislamu?

وَلَوْ شَآءَ رَبُّكَ لَءَامَنَ مَن فِي الْأَرْضِ كُلُّهُمْ جَمِيعًا ۚ أَفَأَنتَ تُكْرِهُ النَّاسَ حَتَّىٰ يَكُونُوا مُؤْمِنِينَ ﴿٩٩﴾

100. Na hakuna mtu anayeweza kuamini isipokuwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Naye hujaalia uchafu uwafike wale ambao hawatumii akili zao.

وَمَا كَانَ لِنَفْسٍ أَن تُؤْمِنَ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ ۚ وَيَجْعَلُ الرِّجْسَ عَلَى الَّذِينَ لَا يَعْقِلُونَ ﴿١٠٠﴾

101. Sema: "Tazameni nini yanayotokea katika mbingu na ardhi!" Na ishara (zote hizi), na mionyo (yote hii) haiwafidishii kitu watu wasioamini.

قُلِ انظُرُوا مَاذَا فِي السَّمَٰوَٰتِ وَالْأَرْضِ ۚ وَمَا تُغْنِي الْءَايَٰتُ وَالنُّذُرُ عَن قَوْمٍ لَّا يُؤْمِنُونَ ﴿١٠١﴾

102. Basi wanangoja jingine ila (kuwajia) mfano wa siku za (adhabu zilizowafika) watu waliopita kabla yao? Sema: "Basi ngojeni, mimi (pia) ni pamoja nanyi katika wanaongojea."

فَهَلْ يَنتَظِرُونَ إِلَّا مِثْلَ أَيَّامِ الَّذِينَ خَلَوْا مِن قَبْلِهِمْ ۚ قُلْ فَانتَظِرُوٓا إِنِّي مَعَكُم مِّنَ الْمُنتَظِرِينَ ﴿١٠٢﴾

103. Kisha tukawaokoa Mitume wetu na wale walioamini. Namna hivi. Ni haki kwetu (sisi) kuwaokoa walioamini.

ثُمَّ نُنَجِّي رُسُلَنَا وَالَّذِينَ ءَامَنُوا ۚ كَذَٰلِكَ حَقًّا عَلَيْنَا نُنجِ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٠٣﴾ ع

104. Sema: "Enyi watu! Ikiwa nyinyi mnayo shaka katika dini yangu, basi mimi siwaabudu

قُلْ يَٰٓأَيُّهَا النَّاسُ إِن كُنتُمْ فِي شَكٍّ مِّن

92. Kiwiliwili cha Firauni kilipanda juu baada ya kuvimba humo ndani ya bahari kama dasturi ya mwenye kufa maji. Kilipanda katika hali hiyo ili hao waliokuwa wakimuabudu waone kwa macho yao kuwa hakuwa Mungu chochote, mbona amezama akanywa maji akavimba kama Mbuzi aliyevimba.

93. Mayahudi wote wakiitakidi kuwa atakuja Mtume mwenye hizo sifa za Nabii Muhammad na wakijitapa kuwa akija watamfuata wawe hivi na hivi na hivi. Lakini alipokuja wakamuona walipandwa na hasadi wakakataa kumfuata ila wachache tu.

94. Maneno haya yanaonyesha dhahiri kuwa haya yaliyomo katika Qurani ni sawa na yaliyoandikwa katika vitabu vya Mitume wengine kabla havijaharibiwa—ya haki hayapingani.

96. Tumetaja katika Aya ya 125 ya *Suratul An-Am* vipi Mwenyezi Mungu anawaongoa na vipi anawaachia kupotea. Siyo anajifanyia tu ovyo.

98. Kuonyesha kuwa watu — au mtu — hata wakiwa wabaya vipi, wakirejea kwa muda mfupi tu KABLA ya kufika adhabu, Mwenyezi Mungu atawapokea.

99. Hii ni moja katika chungu ya Aya zinazoonyesha kuwa waongo hao wanaosema kuwa watu

mnaowaabudu (nyinyi) badala ya Mwenyezi Mungu anayekufisheni. (Basi na nyinyi muabuduni huyo mwenye ufalme huo wa kuhuisha na kufisha). Na nimeamrishwa niwe miongoni mwa wanaoamini ''

دِيْنِيْ فَلَآ اَعْبُدُ الَّذِيْنَ تَعْبُدُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ
وَلٰكِنْ اَعْبُدُ اللّٰهَ الَّذِيْ يَتَوَفّٰىكُمْ ۖۚ وَاُمِرْتُ اَنْ
اَكُوْنَ مِنَ الْمُؤْمِنِيْنَ ۙ (١٠٤)

105. Na (nimeambiwa) "Elekeza uso wako katika dini kwa kumsafishia ibada Mwenyezi Mungu wala usiwe miongoni mwa washirikina. (Basi mimi nafuata, nanyi fuateni).

وَاَنْ اَقِمْ وَجْهَكَ لِلدِّيْنِ حَنِيْفًا ۚ وَلَا تَكُوْنَنَّ
مِنَ الْمُشْرِكِيْنَ (١٠٥)

106. Na (nikaambiwa) 'Wala usiwaabudu badala ya Mwenyezi Mungu wale ambao hawakufai (unapowaabudu) wala hawakudhuru (unapowaacha kuwaabudu). Basi ukifanya, utakuwa miongoni mwa madhalimu (wa nafsi zao)'."

وَلَا تَدْعُ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ مَا لَا يَنْفَعُكَ وَلَا
يَضُرُّكَ ۚ فَاِنْ فَعَلْتَ فَاِنَّكَ اِذًا مِّنَ
الظّٰلِمِيْنَ (١٠٦)

107. Na kama Mwenyezi Mungu akikugusisha dhara, basi hakuna yoyote awezaye kuiondoa isipokuwa yeye (Mwenyewe). Na kama akikutakia kheri, basi hakuna awezaye kurudisha fadhila zake (Mwenyezi Mungu). Huzifikisha (fadhila hizo) kwa amtakaye katika waja Wake (maadamu anajinyenyekeza kwake). Naye ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

وَاِنْ يَّمْسَسْكَ اللّٰهُ بِضُرٍّ فَلَا كَاشِفَ لَهٗٓ اِلَّا
هُوَ ۚ وَاِنْ يُّرِدْكَ بِخَيْرٍ فَلَا رَآدَّ لِفَضْلِهٖ ۗ
يُصِيْبُ بِهٖ مَنْ يَّشَآءُ مِنْ عِبَادِهٖ ۗ وَهُوَ
الْغَفُوْرُ الرَّحِيْمُ (١٠٧)

108. Sema: "Enyi watu! Haki imekwisha kukujieni kutoka kwa Mola wenu. Basi anayeongoka anaongoka kwa (faida ya) nafsi yake, na anayepotea anapotea kwa (khasara ya) nafsi yake (mwenyewe). Na mimi si mlinzi juu yenu (Mimi ni mtoaji khabari tu)."

قُلْ يٰٓاَيُّهَا النَّاسُ قَدْ جَآءَكُمُ الْحَقُّ مِنْ رَّبِّكُمْ ۚ
فَمَنِ اهْتَدٰى فَاِنَّمَا يَهْتَدِيْ لِنَفْسِهٖ ۚ وَمَنْ ضَلَّ
فَاِنَّمَا يَضِلُّ عَلَيْهَا ۚ وَمَآ اَنَا عَلَيْكُمْ
بِوَكِيْلٍ (١٠٨)

109. Na (nimeambiwa): "Fuata yanayofunuliwa kwako (unayoletewa Wahyi). Na vumilia mpaka Mwenyezi Mungu atoe hukumu yake. Naye ndiye bora kuliko mahakimu (wote)."

وَاتَّبِعْ مَا يُوْحٰٓى اِلَيْكَ وَاصْبِرْ حَتّٰى يَحْكُمَ
اللّٰهُ ۚ وَهُوَ خَيْرُ الْحٰكِمِيْنَ (١٠٩) ع

---

wanalazimishwa kuingia katika dini ya Uislamu. Na moja katika hizo ni Aya ya 256 ya *Suratul Baqarah*. Hayo wanayoyasema wanayasema kwa uwongo, na hali ya kuwa wanajua kuwa ni uwongo. Lakini "Akutukanaye hakuchagulii tusi."

100. Kama tulivyosema katika Aya ya 25 na ya 96 ya Sura hii hii.

102. Ukimuona mwenziyo amenyolewa kwa jambo hilo hilo unalolifanya, basi kitie maji upesi kichwa chako kwani na wewe utanyolewa kama alivyonyolewa.

104-107. Zinatajwa hapa kawaida kubwa za kuitakidi na kufuata ndipo uwe Muislamu wa kweli.

109. Mambo ya kustahamili na kustahamiliana yamekaririwa mara nyingi kabisa.

اٰياتها ١٢٣ (١١) سُوْرَةُ هُوْدٍ مَّكِّيَّةٌ (٥٢) رُكُوْعَاتُهَا ١٠

*Ina Aya 123* *Ina Makara 10*

# SURAT HUD

*(Imeteremka Makka)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

1. Alif Lam Ra. Hiki ni Kitabu ambacho Aya zake zimetengenezwa vizuri, kisha zikapambanuliwa (vyema) kutoka kwa (Mwenyezi Mungu) Mwenye hikima na Mwenye ujuzi wa kila kitu

الٓرٰ كِتٰبٌ اُحْكِمَتْ اٰيٰتُهٗ ثُمَّ فُصِّلَتْ مِنْ لَّدُنْ حَكِيْمٍ خَبِيْرٍ ﴿١﴾

2. (Imefanywa hivi) ili msiabudu isipokuwa Mwenyezi Mungu. Hakika mimi kwenu ni muonyaji na mtoaji wa khabari njema ninayetoka kwake

اَلَّا تَعْبُدُوْٓا اِلَّا اللّٰهَ ۭ اِنَّنِيْ لَكُمْ مِّنْهُ نَذِيْرٌ وَّبَشِيْرٌ ﴿٢﴾

3. Na ili muombe msamaha kwa Mola wenu, kisha mtubie (mrejee) Kwake. Atakustareheshení kwa starehe nzuri mpaka muda maalumu (mtapoondoka ulimwenguni). Na atampa (Akhera) kila mwenye fadhila, fadhila yake. Na kama mtakengeuka basi nakukhofieni adhabu ya (hiyo) siku kubwa.

وَّاَنِ اسْتَغْفِرُوْا رَبَّكُمْ ثُمَّ تُوْبُوْٓا اِلَيْهِ يُمَتِّعْكُمْ مَّتَاعًا حَسَنًا اِلٰٓى اَجَلٍ مُّسَمًّى وَّيُؤْتِ كُلَّ ذِيْ فَضْلٍ فَضْلَهٗ ۭ وَاِنْ تَوَلَّوْا فَاِنِّىْٓ اَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ كَبِيْرٍ ﴿٣﴾

4. Marejeo yenu ni kwa Mwenyezi Mungu. Naye ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.

اِلَى اللّٰهِ مَرْجِعُكُمْ ۚ وَهُوَ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيْرٌ ﴿٤﴾

5. Sikilizeni! Wao wanaficha vilivyo vifuani mwao ili wamfiche Mwenyezi Mungu (asiwatambue). Sikilizeni! Wanapojigubika nguo zao naye anajua wanayoyaficha na wanayoyadhihirisha. Hakika Yeye ni Mjuzi wa (hata) yaliyomo vifuani.

اَلَآ اِنَّهُمْ يَثْنُوْنَ صُدُوْرَهُمْ لِيَسْتَخْفُوْا مِنْهُ ۭ اَلَا حِيْنَ يَسْتَغْشُوْنَ ثِيَابَهُمْ ۙ يَعْلَمُ مَا يُسِرُّوْنَ وَمَا يُعْلِنُوْنَ ۚ اِنَّهٗ عَلِيْمٌۢ بِذَاتِ الصُّدُوْرِ ﴿٥﴾

6. Na hakuna nyama yoyote (yaani kiumbe chochote) katika ardhi ila riziki yake iko juu ya Mwenyezi Mungu. Na anajua makao yake ya milele na mahali pake pa kupita tu. (Napo ni hapa duniani). Yote yamo katika Kitabu kinachodhihirisha (kila kitu. Kitabu chake Mwenyezi Mungu anachokijua Mwenyewe hakika yake, si kama vitabu tunavyovijua sisi).

وَمَا مِنْ دَاۗبَّةٍ فِي الْاَرْضِ اِلَّا عَلَى اللّٰهِ رِزْقُهَا وَيَعْلَمُ مُسْتَقَرَّهَا وَمُسْتَوْدَعَهَا ۭ كُلٌّ فِيْ كِتٰبٍ مُّبِيْنٍ ﴿٦﴾

---

3. Kutubia ni kurejea. Na kurejea kwa Mwenyezi Mungu ni kujiepusha na makatazo Yake na kufanya maamrisho Yake. Na imetajwa jaza utakayoipata duniani na Akhera kwa kufanya haya.

6. Muradi wa neno hili "Riziki yake iko juu ya Mwenyezi Mungu" ni kuwa Mwenyezi Mungu amekipa kila kitu ujuzi wa kujitafutia riziki yake kama alivyosema katia Aya ya 2 na ya 3 za *Suratul A'laa* kuwa: "Aliyeumba kila kitu na akakitengeneza. Na akakidiria (kila kimoja jambo lake; na akiongoza (kufanya jambo hilo)." Na akasema vile vile katika Aya ya 20 ya *Surat Abasa* "Kisha akamfanyia njia nyepesi (ya kufanya mambo yake)."